Alhamisi Januari 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580474

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

**EWURA** yafuta bei mpya za maji

UKURASA 3



**Mbaroni** kwa tuhuma kukutwa dawa kulevya

UKURASA 3



**Silva ataka kumfikia Ronaldo**

UKURASA 20

# JPM ataka kujiepusha na magonjwa ya ajabu

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WAHAMIAJI WANASWA NDANI YA NYUMBA**

IDARA ya Uhamiaji mkoani Shinyanga imewakamata watu...

UKURASA WA 4

**WAFANYABIASHARA WALILIA VIFO NGURUWE**

WAFUGAJI na wafanyabiashara wa nguruwe na mazao yake...

UKURASA WA 8

**MAENEO 6 YANAYOFAA UWEKEZAJI WA MIWA**

SERIKALI imetangaza maeneo sita nchini yanayofaa kwa...

MAKALA MAALUM

## Uzazi wa mpango waumiza wazazi

UKURASA 11




Rais Dk. John Magufuli akiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani, Waziri wa Madini, Doto Biteko, Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Prof. Dos Santos Silayo na viongozi wengine wakati akizindua shamba la miti Butengo Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store

# Mfugaji adaiwa kujinyonga sababu mifugo kutaifishwa

UKURASA 2

**MICHEZO** **MGOSI AIANDALIA ZAWADI YANGA PRINCESS** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Wahamiaji haramu wanaswa ndani ya nyumba ya tembe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Shinyanga imewakamata watu 40 wanaodaiwa ni wahamiaji kutoka Ethiopia, waliokuwa wamefichwa kwenye nyumba ya tembe katika kijiji cha Bubiki, Kishapu mkoani hapa.

Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Shinyanga, Rashidi Magetta, alisema hayo juzi mbele ya waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 8:00 usiku na kwamba watu hao walikamatwa wakiwa wamefichwa kwenye nyumba ya Frank Gerald.

Alisema wahamiaji hao haramu kutoka Ethiopia, baada ya kuwahoji walisema wanakwenda Afrika Kusini.

Hata hivyo, alisema ofisi yake bado inawasaka wahamiaji haramu wengine ambao walitoroka kabla ya kukamatwa, ili wakamatwe na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya kuingia nchini kinyume cha sheria za uhamiaji.

Magetta alisema katika mahojiano ya awali, wahamiaji hao walisema kwamba waliingia nchini kwa msaada wa mawakala wanaofanya biashara ya kusafirisha binadamu, mmoja kutoka Kenya na mwingine Mtanzania.

"Tulipokea taarifa za wahamiaji hawa haramu kutoka kwa raia wema kwamba katika kijiji cha Bubiki wilayani Kishapu, kwenye nyumba moja ya tembe, kuna watu wasiofahamika wamehifadhiwa ndani. Tulianza kufuatilia kwa kushirikiana na ofisa mtendaji wa kata ya Bubiki," alisema.

"Katika kufuatilia kwetu, tulifanikiwa kufika kwenye nyumba hiyo na kukuta kundi la watu likiwa limekaa nje usiku huo wa saa 8:00, lakini walipotuona baadhi waliwahi kutawanyika na kukimbia. Tulipoingia ndani ya nyumba tulikuta watu wapatao 40, walibainika ni wahamiaji haramu tukawakamata," aliongeza.

Pia alisema Mtanzania huyo, Frank Gerald, alikimbia baada ya kuona maofisa uhamiaji na sasa anatafutwa huku akibainisha kuwa bado wanaendelea kufanya msako na kudhibiti njia zote za wahamiaji haramu kuingia nchini.

Tukio la kukamatwa kwa wahamiaji haramu hao limekuja siku chache baada ya Rais John Magufuli kutoa msamaha wa bila masharti kwa wahamiaji haramu wapatao 1,789 kutoka Ethiopia ambao sasa watapaswa kuachiwa na kurudishwa nchini kwao.

# JPM ataka kujiepusha na magonjwa ya ajabu

**Na Christina Mwakangale**

RAIS John Magufuli, amewataka Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona kwa kufuata kanuni za kiafya.

Vilevile, amekumbusha umuhimu kwa wananchi kuendelea kumwomba Mungu na kujifukiza ili kukabiliana na virusi hivyo vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19 na kuacha kusikiliza vitisho.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wilayani Chato mkoani Geita wakati wa uzinduzi wa shamba la miti eneo la Butengo, aliloagiza liitwe Shamba la Miti la Silayo.

Aliitaka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia wataalamu wake, kuchukua tahadhari na kuzifanyia uchunguzi baadhi ya chanjo wanazopewa baadhi ya wananchi kabla ya kuanza kutumiwa rasmi.

"Tutaendelea kuchukua tahadhari pamoja na kujifukiza, kusali, kuswali, huku tukiendelea na shughuli zetu, ule vizuri ushibe ili corona inapotaka kuja, ikute mwili uko imara, corona ishindwe na kulegea," alisema.

Rais Magufuli alisema wizara ya afya izingatie matumizi ya chanjo, akitahadharisha kwamba chanjo ya Covid-19 ambayo imeanza kutolewa katika baadhi ya mataifa, huenda isisaidie nchini.

"Katika kipindi hiki ambacho nchi nyingi duniani kutokana na corona wananchi wake wamejifungia ndani, sisi Watanzania hatujajifungia ndani na hatutegemei kujifungia ndani, na wala sitegemei kutangaza hata siku moja kwamba tunajifungia ndani.

"Mungu wetu yupo hai na anaendelea kutulinda, lakini tutaendelea kuchukua tahadhari zingine za kiafya ikiwa ni pamoja na kujifukiza huku unamwomba Mungu.

"Mtatishwa sana ndugu zangu Watanzania, lakini simameni imara. Kuna waliokwenda nje ya nchi na ni Watanzania, wamepatiwa chanjo hiyo ya corona na kurudi nchini wakiwa na virusi hivyo, tena aina mpya. Simameni imara, chanjo hizo hazifai.

"Watanzania hapa wameondoka ndani ya nchi na kukimbilia maeneo mengine na kwenda kuchanjwa na walivyochanjwa, wakaja huku wakatuletea corona ya ajabu ajabu," Rais Magufuli alisema.

Alisema kwamba iwapo corona ingekuwa na chanjo, magonjwa sugu ambayo yamesumbua dunia kwa muda mrefu ikiwamo saratani, UKIMWI, Kifua Kikuu (TB), yangepata chanjo.

""Tusiwe tunakimbilia masuala ya chanjo chanjo, si kila chanjo ina faida kwetu, ni lazima Watanzania tuwe macho, tuwe waangalifu, tutafanyiwa majaribio, tuendelee kumwomba Mungu wetu na tuendelee kuchukua tahadhari, wizara ijiridhishe," alionya.

Kuhusu shamba hilo la miti, Rais Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Wakala wa Misitu (TFS), umeanzisha mashamba mengine manne na kuwa jumla ya mashamba 23.

"Sikutegemea kukutana na misitu na miti ya aina hii mizuri. Kutokana na kazi kubwa aliyoifanya Kamishna wa Misitu, kuanzia leo shamba liitwe 'Silayo Forest'.

"Prof. Dos Santos Silayo! Mamlaka hayo ninayo, sasa litaitwa Shamba la Miti Silayo, ili iwe kumbukumbu kwamba mtu ukifanya kazi nzuri, unakumbukwa," alisema.

WAZIRI NDUMBARO

Awali, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema sekta ya misitu inachangia uchumi wa taifa na kwamba kwa miaka mitatu zimepatikana Sh. bilioni 373 katika sekta hiyo.

Alisema shamba hilo ambalo lilianzishwa mwaka 1954 likiwa sehemu ya shamba la Biharamulo, akisema ni shamba la pili kwa ukubwa kwa misitu Tanzania.

"Misitu ni katika ya chanzo cha fedha na uchumi wa taifa. Halmashauri ikiwamo ya Mafinga inanufaika na misitu ikipata Sh. bilioni 1.3 kwa mwaka. Sasa neema imehamia Chato. Na likikamilika, ajira zitakuwa ni 30,000 ya waliopo eneo hili," alisema.



Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, akimfanyia uchunguzi wa afya nguruwe katika moja ya mabanda yaliyoko wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, juzi. Prof. Nonga alikwenda wilayani humo kwa ajili ya kuongeza nguvu kwa timu iliyoundwa na serikali kwa ajili ya kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa homa ya nguruwe uliyoikumba wilaya hiyo. . **PICHA ; MPIGA PICHA WETU**

# Mfugaji adaiwa kujinyonga sababu mifugo kutaifishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

OPERESHENI ya kuwaondoa wafugaji waliovamia bonde la Ihefu lililoko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Mbarali mkoani Mbeya, imeanza kuleta madhara kwa wafugaji hao baada ya mmoja wao kujinyonga kutokana na ng'ombe wake zaidi ya 50 kukamatwa.

Pawa Kandago (22) mkazi wa Kijiji cha Mapogoro, anadaiwa kuwa alijinyonga kandokando ya hifadhi jirani na mahali mifugo yake ilipochukuliwa na vikosi vya Ulinzi na Usalama vilivyokuwa vinaendesha operesheni hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mazishi ya kijana huyo, Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Lazaro Njogoro, alisema baada ya kuona kijana huyo hapatikani, waliamua kuanza kufuatilia alikokuwa anachunga mifugo hiyo.

Ngojoro alisema inaonekana kijana huyo baada ya kuona mifugo yake imechukuliwa, aliamua kwenda kwenye kichaka na kuamua kujinyonga kwa kutumia mgorole aliokuwa ameuvaa.

"Alipanda kwenye mti na akajifunga lile gorole lake alilokuwa amevaa. Sasa wakati tunamtafuta tuliambiwa na baadhi ya watu kuwa wameona mtu amejinyonga sehemu na tulipokwenda ndipo tukamkuta," alisema Njogoro. Baba wa marehemu, Ng'wandu Sama, alisema mifugo yote aliyokuwa anachunga kijana huyo ilichukuliwa na vikosi vya ulinzi na usalama vya mkoa vilivyokuwa vinaendesha operesheni hiyo ya kuondoa mifugo kwenye hifadhi.

Alisema mifugo hiyo mpaka sasa inashikiliwa, hivyo anaiomba serikali imsaidie arejeshewe na kwamba yuko tayari kulipa faini yoyote atakayotakiwa kuilipa kwa mujibu wa sheria.

Sama alisema kijana huyo ameacha mke na watoto wawili, hivyo anaamini kuwa malezi ya watoto hao yatakuwa magumu endapo mifugo hiyo haitaachiwa.

"Naiomba serikali inisaidie nirudishiwe mifugo yangu, mwanangu amekufa, lakini mifugo yangu pia inashikiliwa maliasili. Kwa kweli hili linaniumiza sana," alisema Sama.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Matagli Mbigili, alivituhumu vikosi vya majeshi vilivyokuwa vinafanya operesheni kuwa vilikuwa vinaswaga na mifugo ya wananchi iliyokuwa inachungwa nje ya hifadhi.

Alisema baada ya elimu kutolewa na maofisa wa serikali wakiwamo wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, wafugaji waliondoa mifugo yao kwenye hifadhi, hivyo kuvifanya vikosi hivyo kukosa kazi na kuanza kukamata mifugo hata nje ya hifadhi hali ambayo imeanza kuleta madhara.

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni kwa tuhuma za kukutwa dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), inawashikilia wakazi watatu wa Jiji la Dar es Salaam kwa tuhuma za kukutwa na gramu 400 za dawa za kulevya aina ya heroine pamoja na bangi, zikiwa zimehifadhiwa ndani ya mfuko wa nailoni.

Watuhumiwa hao ni Anadhati Mchongeza (20), Emmanuel Msakuzi (23) na Kulwa Shamas (49) ambaye ni balozi wa nyumba 50 katika mtaa wa Juwale, Kunduchi Pwani.

Kamishna Jenerali wa DCEA, James Kaji, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa Januari 22, katika eneo la Kunduchi Pwani Kauzeni jijini Dar es Salaam wakiwa na unga unaodhaniwa kuwa ni dawa za kulevya aina ya heroin.

Kaji alisema maofisa wa DCEA baada ya kufanya upekuzi, walikamata kiasi hicho cha dawa zikiwa zimehifadhiwa ndani ya mfuko wa nailoni.

"Mamlaka inaendelea kuwashikilia watuhumiwa na watafikishwa mahakamani baada ya taratibu za kisheria kukamilika. Kadhalika katika kipindi cha Novemba mpaka Desemba, mwaka jana, DCEA ilifanikiwa kushinda kesi kubwa tatu," alisema Kaji.

Kaji alisema ya kesi ya kwanza ilimhusisha mfanyabiashara maarufu jijini Tanga, Yanga Omari Yanga, maarufu Rais wa Tanga, ambaye alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela, baada ya kukutwa na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin uzito wa gramu 1052.63.

Alisema kesi ya pili ni Mahakama Kuu ilimkuta na hatia Ayubu Kiboko na mkewe Pili Kiboko ambao walihukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin zenye uzito wa gramu 251.25.

"Kesi ya tatu ni raia wawili wa Iran walitiwa hatiani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin zenye uzito wa gramu 111.02 katika Bahari ya Hindi na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela pamoja na kutaifishwa kwa jahazi husika."

Kadhalika, Kaji alisema katika kipindi hicho, DCEA ilifanya operesheni mbalimbali na kufanikiwa kumkamata Kibinda Seleman akiwa na dawa za kulevya aina ya heroin kiasi cha gramu 135.12, kwamba mtuhumiwa huwa ameshafikishwa mahakamani.

Alisema kwa mwaka 2020 DCEA ilifungua vituo vingine vitatu vya kutolea tiba ya Methadone katika mikoa ya Tanga, Bagamoyo na Hospitali ya Tumbi mkoani Pwani.

Pamoja na vituo hivyo, alisema DCEA imeongeza wigo wa upatikanaji wa tiba ya uraibu wa dawa za kulevya kwa kuongoza vituo vingine vitatu vya kutolea tiba ya Methadone jijini Dar es Salaam katika maeneo ya Segerea, Mbagala, Tegeta ambavyo vitaanza kutoa huduma Februari, mwaka huu.

Kaji alisema katika kudhibiti na kuzuia uchepushwaji wa kemikali bashirifu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya, DCEA kwa kushirikiana na maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali imetoa mafunzo kwa wadau wapatao 500, wakiwamo madereva malori, wasimamizi wa shughuli zinazohusu kemikali.

# EWURA yafuta bei mpya za maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza kufuta bei mpya za maji zilizopaswa kutozwa kuanzia Januari, mwaka huu, ili kufanya uchunguzi wa kina kutokana na kukithiri malalamiko ya kubambikiziwa ankra za maji wateja.

Bei hizo zilizofutwa ni ambazo zilikuwa zimeidhinishwa na mamlaka hiyo kwa mwaka 2020/21 na kwa sasa zitaendelea kutozwa zilizokuwapo za mwaka 2018/19.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Godfrey Chibulunje, alisema hivi karibuni kumekuwapo na malalamiko makubwa ambapo kati ya malalamiko yote yanayopokelewa na EWURA katika sekta ya umeme, mafuta, gesi asilia, asilimia 60 ni ya maji.

"Kilio kikubwa kutoka kwa wateja wa huduma za maji kipo kwenye ankrra za maji ambapo asilimia 75 ya malalamiko yote ni kutokubaliana na ankra zinazotolewa na mamlaka mbalimbali nchini," alisema.

Alieleza kuwa malalamiko mengine ambayo ni makubwa na migogoro ya uunganishaji huduma za maji ambapo ni asilimia 13.

"EWURA huidhinisha bei kwa mamlaka za maji kwa miaka mitatu ambapo bei hizo ziliidhinishwa kwa mwaka 2018/19, 2019/20 na 2020/21 na kwa utaratibu wetu kuanzia Januari 2021 mamlaka nyingi zilikuwa zinatarajia kuanza kutumia bei za mwaka 2020/21," alisema.

Alisema kutokana na malalamiko hayo imefuta bei zote ambazo zilitakiwa kuanza kutumika mwezi huu na kuelekeza zitumike bei za mwaka 2018/19.

"Hatua hii inachukuliwa ili kuipa uwezo EWURA kufanya uchunguzi wa kina juu ya malalamiko haya ya maji ili kubaini ukweli wa malalamiko hayo, ambapo baada ya kumaliza shughuli ya uchunguzi wa kiufundi, EWURA itatoa maelekezo mengine ya matumizi ya bei ambazo zilitakiwa kuanza Januari, 2021," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema jumla ya mamlaka za maji za mikoa, wilaya, mji midogo na miradi mikubwa ya kitaifa 117 iliomba kuidhinishiwa kupandisha ankra za maji, lakini zimesitishiwa na kwa sasa ankra zitakazotumika ni za 2018/19.

Awali, akifafanua mchakato wa uidhinishaji ankra hizo, Chibulunje, alisema EWURA ina jukumu la kupitia gharama kama zina uhalali kwa kulinganisha na gharama za kipindi cha nyuma za mamlaka husika pamoja na mahesabu ya fedha yaliyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG).

Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa mamlaka hiyo, Exaud Maro, alisema bei za maji zinatofautiana kwa mamlaka za maji huku akisema inatokana na gharama za usafirishaji wa maji kutoka kwenye vyanzo vya maji hadi kuwafikia wateja.


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID: NO. ITB/2021/SUP/002**
**FOR THE ESTABLISHMENT OF A FRAME AGREEMENT FOR THE SUPPLY OF DIESEL FUEL – BULK DELIVERY**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers to submit firm offers for establishment of a frame agreement for the supply of diesel fuel – bulk delivery

**2. Eligibility:**

Suppliers duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

**Kindly download the tender documents in the below link:**

**https://drive.google.com/drive/folders/1L-IhJ_1dUospFRkJx-7YdRLUo7fsQIbKW?usp=sharing**

If you fail to access the link, please write to ishobeza@unhcr.org copy ndassa@unhcr.org

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Pre-bid Conference meeting will be held | Monday 08th February 2021 at 1000 hrs EAT |
| Deadline for receiving requests for clarification | Friday 19th February 2021 at 2359 hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Wednesday 03rd March 2021 at 1700 hrs, EAT |

**UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.**



**VisionFund TANZANIA**

**VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED**
**INTERNAL VACANCY: INTERNAL AUDITOR**

**Please refer to the above heading.**

We urgently need to fill one vacancy existing at Head Office as per organization structure. We need staff that has experience in our operations, policies and procedures. If you are confident and interested to join Internal Audit and Investigation Department, please forward your application to People & Culture as detailed below.

**Position: Internal Auditor**
**Reporting to: Head of Internal Audit and Investigation**

**Responsibility:**
- Assist in coordination, monitor and facilitate compliance with VFT-MFB audit policies and procedures as well as with existing laws, rules and regulations.

**Main tasks**
1. Perform audit work in accordance with the approved audit manual and professional standards
2. Carries out the outlined procedures in the internal audit plan
3. Periodically review, appraise and advise accordingly the soundness, adequacy and efficiency of accounting, financial, business operations process, MIS, P&C and other internal controls
4. Perform operational reviews and appraisals on the cost effectiveness and efficiency with which the company resources are employed in all VFT-MFB business processes
5. Performs audit of VFT-MFB assets to ascertain that they are properly recorded and safeguarded from theft, fraud, and misappropriation
6. Performs audits of VFT-MFB's liabilities and ascertains that they are accurate and genuine
7. Provides investigative services as the need arises and if possible recommend changes on policies and procedures arising from the case(s) investigated in order to strengthen VFT-MFB risk management system
8. Submits a written audit reports to the concerned department/Branch or Business center and discusses and documents feedback of the letter; Monitors whether actions to rectify the reported findings acknowledged by the Board Finance and Audit Committee are undertaken promptly
9. Assists in the execution of the external audit as well as in examinations to be conducted by government regulatory agencies
10. Assists the Head of Internal Audit in sensitizing all staff or concerned staff on changes in internal control and audit policies and procedures
11. Reviews VFT-MFB financial records for accuracy and reliability
12. Carries out other duties as assigned by supervisor from time to time

**Education/Experience**
- Bachelor Degree in Accounting
- CPA/ACCA certification or plan to seat for exam will be an added advantage
- Very good knowledge of oral & written English
- Very good analytical & reporting skills
- 3 years' experience in VFT operations

**Special / Personal Abilities**
- Highly developed sense of reliability and correctness
- Very good communication skills and an effective trainer
- Innovative and analytical
- Very good planning skills
- Must have above average skills in using Micro Soft office applications
- Must be a self-starter, highly motivated, organized, and detail-oriented
- Committed Christian

**Mode of Application:**

Address application letter endorsed by your supervisor together with copies of your certificates & CV to Head of People & Culture, P.o. Box 1546 Arusha and email your application to (rkibwana@vftz.co.tz and amganga@vftz.co.tz ) before January 26, 2021. Recruitment process will apply as contained in the People & Culture Policy Manual.

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Mwanza wakikamilisha taratibu za kupatiwa hati za ardhi kabla ya kukabidhiwa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, akiwa katika ziara ya siku moja katika mkoa huo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**.

# Wafugaji, wafanyabiashara walilia serikali vifo nguruwe

**Na Mbaraka Kambona,** KAHAMA

WAFUGAJI na wafanyabiashara wa nguruwe na mazao yake wanaofanya shughuli zao wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wameiomba serikali kuendelea kuchukua hatua za haraka kuudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa homa ya nguruwe ulioikumba wilaya hiyo.

Wamesema kwamba ugonjwa huo umeathiri kwa kiasi kikubwa shughuli zao za kiuchumi.

Wafugaji na wafanyabiashara hao walitoa ombi hilo walipokuwa wakizungumza na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alipokwenda wilayani humo kwa ajili ya kuiongeza nguvu timu iliyoundwa na serikali ya kudhibiti ugonjwa huo.

Walisema kulipuka kwa ugonjwa huo katika Wilaya ya Kahama kumesababisha hasara kubwa kwa wafugaji na wafanyabiashara kwa sababu nguruwe wengi wamekufa, huku biashara ya mazao ya nguruwe hususan uuzaji wa nyama ukizorota kwa kiasi kikubwa.

Wilson Sawa, mmiliki wa baa na muuza nyama ya nguruwe, alisema biashara ya nyama ya nguruwe imekuwa ikisaidia biashara nyingine, lakini tangu kusitishwa, baa nyingi ambazo zinauza nyama ya nguruwe, hazifanyi vizuri.

"Kusitishwa kwa biashara hii kumeathiri uchumi wetu kwa sehemu kubwa, tunaiomba serikali iharakishe kuudhibiti ugonjwa huu na iendelee kufanya tathmini ya maendeleo ya ugonjwa ili kama unapungua waturuhusu tuendelee kufanya biashara," alisema Sawa.

Naye Pendo Emmanuel, mmiliki wa bucha ya nyama ya nguruwe, alisema kabla ya ugonjwa huo kwa siku alikuwa anauza hadi kilo 80 kwa bei ya jumla na rejareja, lakini kwa sasa hakuna biashara anayoifanya.

"Kwa kweli ugonjwa huu umeathiri kwa kiwango kikubwa katika kuendesha maisha yangu, siwezi kupeleka watoto shuleni, tunaiomba serikali ione itakavyoweza kutusaidia ili tuweze kuendesha maisha yetu," alisema Emmanuel.

Frank Kimaro, mfugaji wa nguruwe, alisema kutokuwapo sehemu rasmi ya kuchinjia kumechangia katika kusambaza ugonjwa huo kwa sababu wakati wote wamekuwa wakichinja nguruwe katika maeneo yalipo mabanda yao.

"Ombi langu kwa serikali ituwekee sehemu itakayokuwa maalum kwa ajili ya kuchinja nguruwe wetu... hii itasaidia kudhibiti milipuko ya magonjwa, lakini serikali nayo itapata mapato yake," alisema Kimaro.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, wa Kahama, Anderson Msumba, alisema serikali ipo kazini kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa haraka ili shughuli za ufugaji na biashara ya nguruwe na mazao yake ziweze kuendelea.

Aliongeza kuwa tangu serikali ilipoingilia kati sakata la ugonjwa huo kwa kupeleka timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuungana na wataalamu wa halmashauri, idadi ya vifo imeanza kupungua na anaamini kwa juhudi zinazoendelea ugonjwa huo sio muda mrefu utakoma.

Kwa upande wake, Prof. Nonga pamoja na kutoa elimu ya kina kuhusu hatua za kuchukua katika kudhibiti ugonjwa huo usisambae, pia aliwataka wafugaji na wanaojihusisha na biashara ya nguruwe kuzingatia masharti ya karantini iliyowekwa na serikali, na kwamba atakayekaidi agizo hilo la serikali sheria itachukua mkondo wake.


TEA RESEARCH INSTITUTE OF TANZANIA

**VACANCY ANNOUNCEMENT**

The Tea Research Institute of Tanzania (TRIT) is an autonomous organization representing the Government of Tanzania and the tea industry. Its duty is to support the continued development of the tea industry, both large and small-scale producers, with appropriate high quality, cost effective research and technology transfer. It is funded by both public and private sector and also from time to time by grant aid from willing donors. TRIT have recently joined hands with IDH, CEFA and TSHTDA to form a consortium for implementing a three years project Agricon - Boresha Chai funded by the European Union through Agri-Connect initiative. TRIT invites suitably qualified Tanzanians to fill the following vacant position:-

**LABORATORY QUALITY SUPERVISOR (1 Post)**
The candidate The candidate who will be reporting to the Program Leader – Soil Fertility Management Programme, should be holder of BSc. degree in Laboratory Technology from a recognized University, with at least 2 years of work experience from a reputable organization. Must be conversant with aspects of Quality Control/Management in the laboratory environment and in computer software particularly MS office packages. The applicant should demonstrate supervisory ability.

**Main Duties and Responsibilities**
. To assist in the coordination and guiding the daily operations of the Soils and Plant analytical laboratory,
. To actively participate in selected analysis of samples brought by clients at the laboratory,
. To supervise specific work assigned to the junior laboratory technicians especially for quality assurance,
. To participate in the development and overseeing of quality assurance and quality control protocols for the laboratory operations,
. To support the implementation of activities leading to the International Acredditation of the laboratory, and
. To coordinate, prepare and submit periodic and regular reports on progress of the laboratory operations within TRIT.

**REMUNERATION**
We offer a very attractive and competitive package for the suitably qualified candidates commensurate with qualifications and experience.

**DUTY STATION**
TRIT Soils and Plant Analytical Laboratory is located at Ngwazi Tea Research Station, Mafinga, Mufindi District, Iringa Region on the shores of the scenic Lake Ngwazi

Please send your application and a full CV to:-

The Executive Director,
Tea Research Institute of Tanzania,
P.O. Box 2177, DAR ES SALAAM
Tel: +255 (O) 22 2122033, +255 (O) 22 2113838
Email: tritdsm@trit.or.tz; info@trit.or.tz

**Closing date for receiving applications is 30th January, 2021. Those who have already applied should not re-apply.**


# Mchakato kutafsiri sheria kwa Kiswahili wasisitizwa

**Na Enock Charles**

SERIKALI imesisitiza kuharakisha mchakato wa kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili kutoka lugha ya Kiingereza inayotumika sasa katika sheria hizo, ili kurahisisha uelewa wa wananchi kuhusu sheria hizo.

Aidha, hatua hiyo itarahisisha upatikanaji wa haki ambazo zinaelezwa kutatizwa na matumizi ya lugha ya Kiingereza ambayo haifahamiki vyema wa Watanzania wengi.

Akizungumza katika mkutano wa nchi wanachama wa Mtandao wa Wasaidizi wa Kisheria Afrika Mashariki (EAHPN) ulioanza jijini Dar es Salaam jana, akijumuisha nchi tisa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa haki kwa maendeleo endelevu ya Afrika Mashariki kupitia mchango wa wasaidizi wa kisheria, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geoffrey Pinda, alisema serikali itaharakisha mchakato huo ili kuboresha upatikanaji wa haki.

"Ipo sheria ambayo inasema utasikilizwa kwa Kiswahili, lakini judgement (hukumu) itaandikwa kwa Kiingereza, kwa hiyo hilo tutalifanyia kazi tujaribu kuipa uhuru ili wananchi wetu wapate msaada ambao ni muhimu sana katika kutendewa haki za kisheria," alisema Pinda.

"Kiingereza kimekuwa kikitumika kutolea maamuzi wakati ni asilimia ndogo tu ya wananchi wanaweza kuitafsiri kwa usahihi, hivyo serikali imeanza mkakati wa kutafsiri sheria ili wananchi wazisome na kuzielewa," aliongeza.

Pinda alisema licha ya ugumu wa lugha ya Kiingereza katika utoaji haki, yapo matatizo mengine ikiwamo rushwa na ukabila na kuuleza umuhimu wa kuimarishwa zaidi kwa taasisi za kisheria pamoja na wasaidizi binafsi wa kisheria ili kuondokana na ukandamizaji kwa wananchi wanyonge katika suala la upatikanaji wa haki za kisheria.

"Tanzania tumeamua kupitia upya taasisi zetu kuona namna zinavyofanya kazi ili ziimarishwe na tuzijengee uwezo," alisema Pinda.

Ofisa Mtendaji Mkuu Shirika la Msaada wa Kisheria (LSF), Lulu Mwanakilala, alisema ni muhimu kwa Watanzania kuzipitia na kuzifahamu sheria mbalimbali za nchi mapema kuliko kusubiri kuja kuzifahamu baada ya kupatwa na matatizo kwa kuwa hiyo itawasaidia kujua haki na wajibu wao.

Alisema wao kama taasisi wanajitahidi kuhakikisha wanawafikia wananchi wengi kwa kadri iwezekanavyo hasa wasio na uwezo ili kuwapa usaidizi wa kisheria.

# TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA - NMB BANK PLC

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

NMB Karibu yako

**Trilioni 4.1** Mikopo Halisi Iliyopo

**Trilioni 7.1** Jumla ya Mali

**Trilioni 5.2** Amana za Wateja

**Faida** kabla ya Kodi ya Mapato **Bilioni 295.4** **40%** YoY

**Faida** Baada ya Kodi ya Mapato **Bilioni 205.5** **45%** YoY

Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa **20%**

Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi **5%**

Uwiano wa Matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi **51%**

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2020 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2020 | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2020 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2020 |
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 661,689 | 457,008 | 661,689 | 457,008 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 385,799 | 536,825 | 385,799 | 536,825 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,304,252 | 1,182,463 | 1,304,252 | 1,182,463 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 129,354 | 335,417 | 129,354 | 335,417 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 238 | 3,836 | 238 | 3,836 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 298 | - | 298 | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 41,474 | 32,218 | 41,474 | 32,218 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 4,109,260 | 3,926,473 | 4,109,260 | 3,928,199 |
| 12 | Mali Nyingine | 206,480 | 197,810 | 278,406 | 355,391 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 2,920 | 2,920 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 215,713 | 217,749 | 181,560 | 183,103 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **7,057,477** | **6,892,719** | **7,095,250** | **7,017,380** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 55,604 | 40,030 | 55,604 | 40,030 |
| 18 | Amana za Wateja | 5,211,056 | 5,203,114 | 5,211,061 | 5,204,607 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 36,645 | 40,792 | 36,645 | 40,792 |
| 20 | Amana Maalumu | 4,188 | 12,985 | 4,188 | 12,985 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,118 | 2,119 | 2,118 | 2,119 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 62,122 | 69,601 | 60,907 | 69,134 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | 295 | - | 295 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | 36,831 | 35,428 | 36,831 | 35,428 |
| 27 | Dhima Nyingine | 73,995 | 72,901 | 111,049 | 196,755 |
| 28 | Madeni | 447,478 | 345,965 | 447,478 | 345,965 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **5,930,037** | **5,823,230** | **5,965,881** | **5,948,110** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **1,127,440** | **1,069,489** | **1,129,369** | **1,069,270** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 896,473 | 896,473 | 903,341 | 903,341 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 206,862 | 148,519 | 205,504 | 145,013 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 524 | 916 | 524 | 916 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,581 | 3,581 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **1,127,440** | **1,069,489** | **1,129,369** | **1,069,270** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 624,882 | 507,684 | 624,882 | 507,684 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 231,287 | 274,736 | 231,287 | 274,736 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 204,809 | 228,308 | 204,809 | 228,308 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 10,055 | 8,674 | 10,055 | 8,674 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 16% | 16% | 15% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5% | 7% | 5% | 7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 81% | 78% | 81% | 78% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 58% | 57% | 58% | 56% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79% | 79% | 78% | 78% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0% | -4% | 0% | -5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2% | -3% | 1% | -3% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo ya Mwaka sasa 31.12.2020 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 | Robo ya Mwaka sasa 31.12.2020 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 |
| 1 | Mapato ya Riba | 197,565 | 163,031 | 197,596 | 163,265 | 712,647 | 653,195 | 712,976 | 653,974 |
| 2 | Gharama za Riba | (34,461) | (31,229) | (34,461) | (32,607) | (139,201) | (130,820) | (139,201) | (136,333) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **163,104** | **131,803** | **163,135** | **130,658** | **573,446** | **522,375** | **573,775** | **517,641** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - | - | (1,621) | - | (1,621) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (38,313) | 3,052 | (38,313) | 3,052 | (119,312) | (98,789) | (119,312) | (98,789) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **76,263** | **64,508** | **76,263** | **64,508** | **266,241** | **204,409** | **266,242** | **204,409** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 10,002 | 5,174 | 10,002 | 5,174 | 28,638 | 24,453 | 28,638 | 24,453 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 63,598 | 55,456 | 63,598 | 55,456 | 225,988 | 169,134 | 225,989 | 169,134 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - | 17 | 31 | 17 | 31 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 2,663 | 3,878 | 2,663 | 3,878 | 11,598 | 10,791 | 11,598 | 10,791 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(115,663)** | **(102,127)** | **(113,549)** | **(102,826)** | **(423,572)** | **(410,513)** | **(425,260)** | **(410,552)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (56,207) | (49,388) | (56,207) | (49,388) | (210,175) | (198,713) | (210,175) | (198,713) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (3,591) | (152) | (3,591) | (152) | (10,603) | (10,793) | (10,603) | (10,793) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (55,865) | (52,587) | (53,751) | (53,286) | (202,794) | (201,007) | (204,482) | (201,046) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **85,390** | **97,236** | **87,536** | **95,392** | **296,803** | **215,861** | **295,445** | **211,088** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (27,045) | (28,424) | (27,045) | (28,424) | (89,941) | (71,122) | (89,941) | (68,921) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **58,345** | **68,812** | **60,491** | **66,968** | **206,862** | **144,739** | **205,504** | **142,167** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | | | | | |
| | **Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa** | **(391)** | **10** | **(391)** | **10** | **(525)** | **168** | **(525)** | **168** |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **57,954** | **68,822** | **60,100** | **66,978** | **206,337** | **144,907** | **204,979** | **142,335** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,465 | 3,450 | 3,465 | 3,450 | 3,465 | 3,450 | 3,465 | 3,450 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 117 | 138 | 121 | 134 | 414 | 289 | 411 | 284 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 226 | 224 | 226 | 224 | 226 | 224 | 226 | 224 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Mali | 3% | 4% | 3% | 4% | 3% | 2% | 3% | 2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 21% | 28% | 23% | 28% | 18% | 15% | 20% | 15% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 48% | 52% | 47% | 53% | 50% | 56% | 51% | 57% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12% | 11% | 12% | 11% | 10% | 11% | 11% | 11% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2020 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2020 | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2020 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 85,390 | 75,471 | 87,536 | 74,241 | 296,803 | 215,861 | 295,445 | 211,088 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 10,309 | 9,665 | 9,816 | 9,172 | 43,993 | 73,367 | 42,022 | 73,609 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (192,043) | (136,096) | (190,317) | (134,779) | (560,728) | (348,605) | (555,046) | (343,894) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | (131) | - | (131) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 10,572 | (249,191) | 9,084 | (250,575) | 379,104 | 614,007 | 373,382 | 607,347 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | (2,717) | - | (2,717) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (5,280) | (6,905) | (92,826) | (9,811) | 2,573 | 36,843 | (91,160) | 54,422 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,591 | 95,587 | 88,246 | 100,283 | 45,302 | (21,716) | 142,404 | (36,876) |
| - Kodi Iliyolipwa | (35,006) | (24,971) | (35,006) | (24,971) | (122,088) | (60,418) | (122,088) | (56,357) |
| - Mengineyo (bainisha) | 10,472 | (30,545) | 10,472 | (30,545) | 11,964 | 10,063 | 11,964 | 10,063 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(112,995)** | **(266,985)** | **(112,995)** | **(266,985)** | **96,923** | **516,554** | **96,923** | **516,554** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (8,272) | (5,114) | (8,272) | (5,114) | (22,397) | (12,649) | (22,397) | (12,649) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | 292 | - | 292 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | (659,892) | - | (659,892) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | 641,480 | - | 641,480 |
| Mengineyo (bainisha) | (122,182) | (214,054) | (122,182) | (214,054) | (543,222) | (10,967) | (543,222) | (10,967) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(130,454)** | **(219,168)** | **(130,454)** | **(219,168)** | **(565,619)** | **(41,736)** | **(565,619)** | **(41,736)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - | (48,000) | (33,000) | (48,000) | (33,000) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 101,513 | (29,475) | 101,513 | (29,475) | 100,035 | (71,102) | 100,035 | (71,102) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | (60) | - | (60) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **101,513** | **(29,475)** | **101,513** | **(29,475)** | **52,035** | **(104,162)** | **52,035** | **(104,162)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(141,936)** | **(515,628)** | **(141,936)** | **(515,628)** | **(416,661)** | **370,656** | **(416,661)** | **370,656** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 938,645 | 1,454,273 | 938,645 | 1,454,273 | 1,213,370 | 842,714 | 1,213,370 | 842,714 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **796,709** | **938,645** | **796,709** | **938,645** | **796,709** | **1,213,370** | **796,709** | **1,213,370** |

## TAARIFA YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **944,473** | **-** | **-** | **4,630** | **969,103** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 206,862 | - | - | - | 206,862 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (525) | (525) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,103,335** | **-** | **-** | **4,105** | **1,127,440** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **799,129** | **-** | **33,725** | **4,342** | **857,196** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 144,619 | - | - | 120 | 144,739 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 168 | 168 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 33,725 | - | (33,725) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **944,473** | **-** | **-** | **4,630** | **969,103** |

## TAARIFA YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **951,341** | **-** | **-** | **1,049** | **972,390** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 205,504 | - | - | - | 205,504 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (525) | (525) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,108,845** | **-** | **-** | **524** | **1,129,369** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **808,449** | **-** | **33,725** | **881** | **863,055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 142,167 | - | - | - | 142,167 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 168 | 168 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 33,725 | - | (33,725) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **951,341** | **-** | **-** | **1,049** | **972,390** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA DISEMBA 2020

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna **Afisa Mtendaji Mkuu** | | Januari 25, 2021 |
| Benedicto Baragomwa **Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha** | | Januari 25, 2021 |
| Juma Kimori **Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | Januari 25, 2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede **Mwenyekiti wa Bodi** | | Januari 25, 2021 |
| Leonard Mususa **Mkurugenzi** | | Januari 25, 2021 |

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tujihadhari na corona

**JANA** Rais John Magufuli aliwataka Watanzania kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona, kwa kuwa nchi zinazotuzunguka zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na Tanzania siyo kisiwa.

Rais alisema katika kipindi hiki ambacho kuna magonjwa yanajitokeza yayasiyojulikana kama corona, nchi nyingi wananchi wake watakuwa wamejifungia ndani, Watanzania hawajajifungia na hawategemei kujifungia, na hatatangaza kwamba Watanzania wanajifungia kwa sababu Mungu yupo hai na ataendelea kutulinda.

Aidha, alisema ni muhimu kuchukua tahadhari zingine za kiafya ikiwamo kujifukiza, maombi, mazoezi na kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya.

Alisema Watanzania watatishwa sana katika kipindi hiki, lakini ni muhimu kusimamia imani, huku wananchi walikimbilia nje ya nchi kwenda kuchanjwa na wameleta ugonjwa.

Aidha, amesisitiza kuwa chanjo bado haifai, na kwamba bado saratani, malaria na Ukimwi havina chanjo, huku akiwataka wananchi kuwa waangalifu na mambo ya kuletewa na wasifikiri wanapendwa sana, huku akitahadharisha Wizara ya Afya kutokimbilia chanjo kabla ya kujiridhish.

Kwamba siyo kila chanjo ni ya maana kwa taifa na inafaida kwa nchi bali kinachotakiwa ni uangalifu ili kuepuka kufanyiwa majaribio.

Tahadhari hiyo inakuja siku chache baada ya Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Arusha, Askofu Isaac Amani, kutaka wananchi kurudi katika utamaduni wa kunawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni, kukaa umbali na kuwataka waumini kutomjaribu Mungu kwa kufanya uzembe ambao ameufananisha na kutembea pekupeku juu ya mbigili.

Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Yuda Thaddeus Ruwa'ichi, aliwataka waumini kutojidanganya na kuchukua tahadhari zote muhimu za kujikinga kwa kuwa ugonjwa huo bado unazitesa nyingi nyingi duniani.

Aidha, Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga, aliwataka waumini kuchukua tahadhari zote muhimu za kujikinga na janga hilo.

Alisema nchi kadhaa zimethibitisha kuwa zinapitia kipindi kigumu cha kueneo kwa corona na kutokea vifo vya watu, na kwamba Tanzania siyo kisiwa ni lazima kuzingatia hekima za wahenga kuwa mwenzio akinyolewa wewe tia maji.

Nasi tunaungana na wote wanaoona hatari iliyopo nchini na kutoa tahadhari muhimu sana kwa kuwa corona inazitesa nchi nyingi na mamia ya watu wameshapoteza maisha na wanaendelea kufa.

Tunasema ni muhimu sana kuchukua tahadhari muhimu zilizoelekezwa na wataalam wa afya kama kukaa kwa umbali, kunawa mikono mara kwa mara na vitakasa mikono, kuepuka misongamano na kuvaa barakoa.

Machi mwaka huu, ugonjwa huo ulivyotangazwa kuingia nchini na shule kufunguliwa ulitolewa mwongozo wa namna ya kuishi kwenye shule na vyuo taratibu ambazo ziliachwa baada ya muda mfupi na watu kurudi katika maisha kama kawaida, na katika sehemu za huduma muhimu za kijamii kama hospitali wananchi hawakuruhusiwa kuingia bila kuvaa barakoa na kunawa mikono.

Katika nyumba za ibada baadhi ya taratibu zilibadilishwa kama kusalimiana kwa kushikana mikono, kupata mkate wa bwana kwa kulishwa na kunawa maji ya baraka , huku kukiwa na utaratibu wa kunawa mikono kabla na wakati wa kutoka katika nyumba hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hili hapa shamba la miti Silayo, alilolibatiza JPM

**JANA** kulikuwapo uamuzi wa kihistoria nchini, Rais Dk. John Magufuli, alipozindua Shamba la Miti Silayo, ambalo kabla, liliitwa Shamba la Miti la Chato, katika eneo la Butengo, wilayani Chato mkoani Geita.

Hapo lina ukubwa wa hekta 69,000 na la pili kwa ukubwa nyuma ya Shamba la Miti Sao Hill, lililopo Mafinga mkoa wa Iringa lenye hekta 135,900.

Dk. John Magufuli, alibadili jina hilo jana katika tukio lililohudhuriwa na viongozi mbalimbali, akiwamo Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro na naibu wake, Mary Masanja na Waziri wa Nishati, Medard Kalemani.

Pia alikuwapo Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Do Santos Silayo, ambaye jina lake limeenziwa, kwa ubunifu na kuuwezesha mradi huo.

Ni mara ya pili Dk. Magufuli, kuenzi mradi kwa kulipa jina la aliyeufanikisha. Wa kwanza ni Mhandisi Patrick Mfugale, aliyewezesha Daraja la Mfugale, jijini Dar es Salaam.

Hatua ya kuanzisha shamba hilo, inaanzia kutoka hatua za uharibifu mkubwa uliofanywa na wananchi jirani waliopavamia na ndipo serikali kupitia TFS, ikaamua kupaendeleza.

Lengo hapo ni kutunza mazingira sasa ikiwa katika wasifu wa sura nyingi kama shamba, mlinzi wa mazingira, mradi kiuchumi na kivutio cha utalii.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, anasema ni mradi unaotarajiwa kifanikisha upandaji miti na kutoa mchango mkubwa katika kuhifadhi mazingira na ndani ya Kanda ya Ziwa.

**Tangu kuanzishwa kwa shamba hilo, hadi sasa imeshapanda miti migumu na laini, ukiwamo mkongo kwenye eneo la ukubwa wa hekta 522, sawa na miti 579,942, sawa na asilimia moja ya eneo lote la shamba**

Anafafanua kuwa shamba hilo lilianzishwa kukabili uharibifu mkubwa wa shughuli za kibinadamu katika Hifadhi ya Msitu wa Biharamulo- Kahama, hasa katika eneo la Chato, kati ya mwaka 2017 na 2018.

"Tangu kuanzishwa kwa shamba hilo, hadi sasa imeshapanda miti migumu na laini, ukiwamo mkongo kwenye eneo la ukubwa wa hekta 522, sawa na miti 579,942, sawa na asilimia moja ya eneo lote la shamba," anasema Mkuu wa Mkoa.

Waziri wa Nishati, Medard Kalemani, anasema kuna miti 85,000 aina ya mikaratusi inayotarajiwa kupandwa katika shamba hilo, kwa ajili ya nguzo kufanikisha upatikanaji wa nguzo za umeme na malighafi kwa viwanda kuzalisha karatasi.

Mradi huo anaueleza tangu kuanzishwa umewezesha ajira 600 akiwa na ufafanuzi: "Ajira hizo ni kwa wananchi wanaozunguka shamba na uanzishaji wa bustani yenye zaidi ya miche 900,000, kwani tunaamini kuwa Tanzania ya Viwanda inawezekana, hivyo tupande miti kwa maendeleo ya viwanda."

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, anasema ni shamba lenye manufaa kitaifa, kwa kuwa ni kivutio cha utalii kando ya Ziwa Victoria, ukanda wenye vivutio vingi vya kutembelewa.

Waziri Dk. Ndumbaro, anaongeza: "Utalii unachangia asilimia 17.5 katika pato la taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni, hivyo kuanzishwa Shamba la Silayo, kutakuwa na faida kwa uchumi wa taifa."

Anaongeza kuwa, shamba hilo litatumika kuzalisha mazao yatokanayo na miti na nyuki ili kukuza uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

**TANGAZO**

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**

*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 11,959 | 10,798 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,900 | 13,814 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 22,770 | 21,550 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 17,178 | 207 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 40 | 37 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 26 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 77,800 | 80,858 |
| 12 | Mali Nyingine | 13,041 | 12,467 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 20 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 15,754 | 20,475 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **172,489** | **160,227** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,511 | 3,587 |
| 18 | Amana za Wateja | 118,304 | 112,757 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 2 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,154 | 4,250 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 7 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazol | 537 | 613 |
| 27 | Dhima Nyingine | 16,503 | 20,245 |
| 28 | Madeni | 713 | 816 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **140,723** | **142,278** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **31,766** | **17,949** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,984 | 10,984 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 3,025 | 586 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (6,617) | (3,442) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 24,374 | 9,820 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **31,766** | **17,949** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 102 | 438 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 19,074 | 17,907 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 11,506 | 9,507 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 18.4% | 11.2% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 20.7% | 19.4% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75.8% | 77.1% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 53.5% | 57.7% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 68.3% | 64.0% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3.0% | 4.2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 7.7% | 3.4% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-20 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 5,445 | 7,770 | 23,917 | 29,265 |
| 2 Gharama za Riba | (2,275) | (2,909) | (7,767) | (6,803) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **3,170** | **4,862** | **16,150** | **22,461** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (2,000) | (421) | (3,886) | (1,824) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,262** | **1,031** | **5,283** | **6,211** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 67 | 97 | 286 | 349 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 913 | 1,061 | 3,689 | 5,039 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 282 | (127) | 1,308 | 823 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,607)** | **(7,406)** | **(24,165)** | **(28,074)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,188) | (4,103) | (13,071) | (14,645) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,420) | (3,302) | (11,094) | (13,428) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(3,175)** | **(1,934)** | **(6,617)** | **(1,226)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | (1,450) | 0 | (1,663) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(3,175)** | **(3,384)** | **(6,617)** | **(2,889)** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(3,175)** | **(3,384)** | **(6,617)** | **(2,889)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 416 | 427 | 416 | 429 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (289) | (308) | (602) | (263) |
| **15 Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -7.6% | -9% | -4.0% | -2% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -51.1% | -60% | -26.6% | -13% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 126.5% | 126% | 112.7% | 98% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11.5% | 17% | 14.7% | 20% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (3,175) | 262 | (6,617) | (1,226) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Hasara Katika Mali | 544 | 645 | 2,657 | 5,604 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,059 | (5,463) | 6,946 | (3,922) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 | 0 | (3) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 3,471 | 4,721 | 9,343 | (7,921) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,220) | 450 | 2,900 | 1,531 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (777) | 272 | (11,436) | (599) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 873 | 225 | (591) | 3,865 |
| - Kodi Iliyolipwa | (1,474) | (7) | (1,897) | 0 |
| - Mengineyo (Kiwango cha chini cha tengo la ziada) | 384 | 419 | 2,298 | 2,208 |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **1,685** | **1,522** | **3,603** | **(463)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (44) | (20) | (133) | (427) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | (0) | 0 |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(44)** | **(20)** | **(133)** | **(424)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 2,377 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | (2) | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (Malipo ya Ukodishaji, tangulizi ya mtaji wa hisa) | 16,353 | (586) | 14,066 | (2,450) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **16,353** | **(586)** | **14,064** | **(73)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 17,994 | 916 | 17,533 | (960) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 18,164 | 17,248 | 18,624 | 19,584 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **36,157** | **18,164** | **36,157** | **18,624** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **-** | **-** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (6,616,805) | - | - | - | **(6,616,805)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,662,764) | 1,662,764 | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 16,992,072 | **16,992,072** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(3,591,929)** | **4,949,707** | **-** | **16,992,072** | **31,766,183** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8,607,135** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **-** | **21,902,271** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (2,888,636) | - | - | - | (2,888,636) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 2,377,281 | - | - | - | - | - | 2,377,281 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (749,687) | 749,687 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 779,217 | - | (779,217) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2019** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **-** | **-** | **21,390,916** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020**

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Juliana Swai<br>**(Kaimu Mtendaji Mkuu)** | ………………….. | 25-Jan-21 |
| Bertha Simon<br>**(Mkuu wa Fedha)** | ………………….. | 25-Jan-21 |
| Chemo Mutani<br>**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | ………………….. | 25-Jan-21 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1. Ernest Massawe | ………………….. | 25-Jan-21 |
| 2. Dr. Josephat Daniel Lotto | ………………….. | 25-Jan-21 |

**Sasa unaweza kulipia malipo yote ya Serikali (GePG) na Kodi za TRA kupitia Akiba Mobile na Matawi yetu yote ambayo hayana foleni."**

# Makandarasi wazalendo wafundwa mikataba

## Maeneo 6 yanayofaa uwekezaji wa miwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetangaza maeneo sita nchini yanayofaa kwa uwekezaji kilimo cha miwa, yenye uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 976,000 za sukari kwa mwaka.

Aidha, imesema haitasita kumruhusu mwekezaji mwingine kujenga kiwanda katika Bonde la Kilombero kutokana na kiwanda kilichopo kushindwa kununua tani 200,000 za miwa iliyopo kwa wakulima wadogo.

Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, aliyasema hayo jana, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzalishaji wa sukari.

Alitaja maeneo hayo ambayo ukubwa wake upo kwenye mabano ni Kibondo (hekta 25,000), Kasulu (hekta 37,000), Rufiji (hekta 25,000), Songwe (hekta 22,000), Mara (hekta 12,000), Mpanda (hekta 27,462), na Rukwa (hekta 12,372).

"Serikali kupitia Bodi ya Sukari na Kituo cha Uwekezaji itaendelea kutangaza maeneo haya kwa ajili ya kupata wawekezaji na kuongeza uzalishaji wa sukari," alisema.

Kuhusu kiwanda cha Kilombero, Waziri alisema moja ya sababu za uwapo wa uhaba wa sukari ni miwa ya wakulima kubaki shambani bila kuvunwa kwa sababu ya ufanisi na uwezo mdogo wa viwanda hususani cha Kilombero.

**Na Joseph Mwendapole**

MAKANDARASI wazalendo wamekumbushwa kusoma mikataba kwa makini na kuielewa kabla ya kuitia saini kwa kuwa kutofanya hivyo kunaweza kuwaingiza kwenye hasara na migogoro.

Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mhandisi Consolata Ngimbwa, alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu kwa zaidi ya makandarasi 100 kuhusu usimamizi wa mikataba.

Alisema imekuwa desturi kwa makandarasi wazalendo kutoisoma mikataba kwa makini ili kubaini kama kuna kasoro na kuifanyia marekebisho lakini wamekuwa wakikurupuka kutia saini na kuishia kupata hasara.

"Unakuta mkandarasi analalamika kwamba hajalipwa, lakini je, mkataba wake unasemaje kuhusu malipo? Unakuja mkataba unatia saini tu unakuja kugundua baadaye kwamba una matatizo unaanza kulia hasara," alisema.

Ngimbwa alisema makandarasi wa nje wamekuwa makini sana kusoma mikataba na kama wanaona kuna kasoro wanazungumza na wateja wao na kuweka mambo sawa tofauti na wazalendo.

"Kama hamuwezi kusoma mikataba, wataalamu wa mikataba wapo wanaweza kuwashauri kama kuna kitu hakiko sawa mkae na mteja mfikie makubaliano ya suala hilo. Hata kama hamkuafikiana unakuwa umejiandaa kwamba kwenye kazi hii kuna hiki na hiki sasa ukishakwama ndipo unakumbuka mkataba ambao tayari umeshaota vumbi kabatini," alisema Ngimbwa.

Mwenyekiti huyo aliwahimiza makandarasi wazalendo kuzingatia umuhimu wa kuungana katika kushiriki zabuni za miradi mikubwa ya ujenzi kwa ubia ili waweze kupata zabuni nyingi.

"Hivi sasa kuna fursa ya ujenzi wa kipande cha reli Mwanza. Hii ni fursa kwenu nendeni mkasikilize hiyo zanuni kwani mnaweza kupata kazi badala ya kukaa hapa na kulalamika kila siku kwamba hampewi fursa," alisema.

"Mjitahidi kutoshiriki vitendo vya rushwa, msitoe wala kushawishi, lakini pia msikubali kushawishiwa kutoa rushwa kwa sababu mkiwa weledi na mahiri katika kazi zenu mtapata kazi bila kutoa rushwa," alisisitiza.

Aliwakumbusha makandarasi wazalendo kuzingatia umuhimu wa kuungana katika kushiriki zabuni za miradi mikubwa ya ujenzi kwa ubia ili waweze kupata zabuni nyingi.

Pia alisema serikali imeonyesha nia ya kuhakiisha ushiriki wa makandarasi wazalendo katika zabuni za miradi mikubwa, lakini watakaopewa kipaumbele ni wale walioijiunga katika ubia.

Alisema serikali ilitenga miradi miwili maalum kwa ajili ya kukuza uwezo wa makandarasi wazalendo ambayo ni ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Kailua-Urambo yenye urefu wa Kilomita 28na Rudewa Kilosa Km 24.

Mafunzo yanayotolewa na bodi hiyo, alisema ni muhimu na yanalenga kuboresha utendaji kazi wa makandarasi kwani kazi hizo zinahusu mikataba ya ujenzi wa miradi mbalimbali.

Mwenyekiti aliwaambia makandarasi kuwa migogoro mingi inayotokea katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi hapa nchini na kwingineko duniani inatokana na kutozingatiwa kwa mikataba husika.

Alibainisha kuwa hali hiyo imekuwa ikisababisha na ukosefu wa uelewa wa mikataba kwa upande mmoja au hata pande zote mbili za mkataba na iwapo pande zote zitaelewa vizuri mikataba basi utekelezaji wa miradi huwe wa mafanikio makubwa.


Bank of India (Tanzania) Ltd.

Relationships beyond banking

Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)

## UONESHAJI WA TAARIFAZA FEDHA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

#### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,758 | 1,677 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,599 | 14,049 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 49,829 | 51,020 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,549 | 1,671 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 18,803 | 20,411 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 70,823 | 72,450 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,572 | 3,067 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,243 | 2,350 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **163,176** | **166,695** |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 53,125 | 57,151 |
| 18 | Amana za Wateja | 68,384 | 68,810 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 28 | 29 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 25 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,773 | 2,363 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,759 | 2,046 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **126,094** | **130,424** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **37,082** | **36,271** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,512 | 3,328 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 9,971 | 10,201 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,099 | 1,242 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **37,082** | **36,271** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 8,720 | 3,280 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,032 | 6,307 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 450 | 2,858 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.73% | 21.76% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.66% | 8.38% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 58.66% | 59.79% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 43.40% | 43.46% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85.74% | 88.03% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -3.53% | 10.29% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -2.11% | 8.01% |

#### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 3,191 | 2,934 | 12,490 | 12,135 |
| 2 Gharama za Riba | 1,295 | 1,226 | 5,014 | 4,889 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,896** | **1,708** | **7,476** | **7,246** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 175 | (2) | 182 | (2) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (274) | 549 | 656 | 709 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **189** | **173** | **697** | **961** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 34 | 35 | 188 | 223 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 155 | 138 | 509 | 738 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,326** | **1,153** | **4,699** | **4,366** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 457 | 419 | 1,743 | 1,642 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 869 | 734 | 2,956 | 2,724 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **858** | **182** | **2,636** | **3,134** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | - | 90 | 537 | 810 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **858** | **92** | **2,099** | **2,324** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya** | **858** | **92** | **2,099** | **2,324** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 30 | 29 | 30 | 29 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 160 | 17 | 98 | 108 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.11% | 0.50% | 1.68% | 2.14% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 9.35% | 1.02% | 5.81% | 6.46% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 39.23% | 37.11% | 35.63% | 33.34% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.39% | 5.25% | 5.58% | 5.49% |

#### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.10.2020** | 21,500 | - | 11,442 | 3,328 | - | - | 36,271 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 858 | - | - | - | 858 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (184) | 184 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | (47) | | | | (47) |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.12.2020** | 21,500 | - | 12,070 | 3,512 | - | - | 37,082 |
| **Robo Mwaka iliyopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.07.2020** | 21,500 | - | 10,677 | 3,457 | - | - | 35,635 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 636 | - | - | - | 636 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 129 | (129) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.09.2020** | 21,500 | - | 11,442 | 3,328 | - | - | 36,271 |

#### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 858 | 636 | 2,636 | 3,134 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | (78) | 439 | 1,406 | 898 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,899 | (1,364) | (2,224) | (975) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (4,452) | 11,753 | 14,351 | (11,696) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 5,039 | (3,917) | (839) | (1,659) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 509 | (21) | (602) | 695 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,826) | (2,161) | (4,131) | (736) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (45) | - | (886) | (810) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za*** | ***1,904*** | ***5,365*** | ***9,710*** | ***(11,150)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (66) | (132) | (215) | (103) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(66)*** | ***(132)*** | ***(215)*** | ***(103)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (387) | - | (387) | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***(387)*** | - | ***(387)*** | - |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **1,451** | **5,233** | **9,108** | **(11,253)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 31,089 | 25,856 | 23,432 | 34,685 |
| | **Robo Mwaka** | **32,540** | **31,089** | **32,540** | **23,432** |

BOI (TANZANIA) LTD
DAR ES SALAAM

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2020**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Ashwani Kumar Negi<br>Mkurugenzi Mkuu | | 21.01.2021 |
| Mr. Heriabdiel Ayoh<br>Mkuu wa Fedha | | 21.01.2021 |
| Mr. Allen Richard<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | | 21.01.2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Dr. Bernard E. Mnzava - Director | | 21.01.2021 |
| 2. Mr. Suitbert Kageuka - Director | | 21.01.2021 |

TANGAZO

# Letshego Bank — LETSHEGO BANK (T) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12. 2020

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka/ Mwaka wa sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 638 | 370 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 6,145 | 6,049 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 331 | 934 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 27 | 15 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo (Baada ya tengo la mikopo) | 28,605 | 28,507 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,099 | 2,107 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,536 | 1,631 |
| 16 | JUMLA YA MALI | 39,382 | 39,613 |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 4,206 | 4,046 |
| 18 | Amana za Wateja | 9,590 | 9,758 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa fedha Islimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbikizo za Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 291 | 364 |
| 24 | Dhima la Tozo Kwaajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Meneja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,438 | 1,344 |
| 28 | Madeni | 6,700 | 10,700 |
| 29 | JUMLA YA DHIMA | 22,225 | 26,212 |
| 30 | MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 20) | 17,157 | 13,400 |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 45,007 | 41,057 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | - | - |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (25,560) | (25,560) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | (2,290) | (2,096) |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa Chache | - | - |
| 37 | JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA | 17,157 | 13,400 |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 90) | - | - |
| 40 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 30) | 4,477 | 4,399 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,240 | 5,599 |
| 42 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 0% | 0% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi (Zaidi ya Siku 90) | 44% | 34% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi (Zaidi ya Siku 30) | 13.6% | 12.9% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 247% | 247% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 86% | 86% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81% | 81% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0% | 7% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1% | 15% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni

| | | Robo ya Mwaka Sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,466 | 1,810 | 6,576 | 7,575 |
| 2 | Gharama za Riba | (488) | (430) | (1,724) | (1,652) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 978 | 1,380 | 4,852 | 5,923 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | (87) | (283) | (1,213) | (5,338) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la Tengo katika Mikopo | 856 | (114) | 1,029 | 4,118 |
| 6 | Mapato yasiyo na Riba | 228 | 316 | 1,073 | 1,568 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (6) | 0 | (11) | 53 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 174 | 233 | 832 | 1,357 |
| | 6.3 Gawio | 0 | - | 0 | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 60 | 83 | 252 | 159 |
| 7 | Gharama Zisizo za Riba | (2,141) | (2,136) | (7,985) | (8,048) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,197) | (1,193) | (4,548) | (4,394) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gawio | (944) | (943) | (3,437) | (3,655) |
| 8 | Faida / (Hasara) ya Uendeshaji | (166) | (836) | (2,244) | 222 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (31) | 0 | (46) | 0 |
| 10 | Faida / (Hasara) Hasili Baada ya Kodi ya Mapato | (197) | (836) | (2,290) | 222 |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 150 | 155 | 150 | 151 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | (0) | 00 | (0) | (0) |
| 13 | Mapato ya Hisa yaliyochujwa | (0) | 00 | (0) | (0) |
| 14 | Idadi ya Matawi | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0% | -2% | 0% | 1% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa fedha za wanahisa | -1% | -5% | -1% | 1% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 126% | 100% | 126% | 88% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazo Zalisha | 2% | 3% | 2% | 16% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.03.2020
(Kiasi kwa shilingi '000)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa Sasa | | | | | | |
| Salio la Mwanzo wa Mwaka | 29,937 | 8,520 | - | - | (25,560) | 12,897 |
| 1 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 6,550 | | | | | 6,550 |
| 2 Mapato Mengine yaliyoainishwa | - | | | | | |
| 3 Miamala na wanahisa | | | | | | |
| 4 Gawio lililolipwa | | | | | | |
| 5 Ziada ya Kisheria | | | | | | |
| 6 Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | | (2,290) | (2,290) |
| 7 Menginevyo | - | - | - | | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 36,487 | 8,520 | - | - | (27,850) | 17,156 |
| Mwaka Uliopita | | | | | | |
| Salio la Mwanzo wa Mwaka | 29,237 | 8,520 | 291 | - | (23,014) | 15,034 |
| 1 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 700 | | | | | 700 |
| 2 Mapato mengine yaliyoainishwa | - | - | - | - | - | - |
| 3 Miamala na Wanahisa | - | - | (291) | - | 291 | - |
| 4 Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| 5 Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| 6 Tengo la Ziada ya Jumla | - | | | - | (2,837) | (2,837) |
| 7 Menginevyo | - | | | | | |
| Salio la Mwisho wa Mwaka | 29,937 | 8,520 | - | - | (25,560) | 12,897 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020
(Amounts in million of shillings)

| | | Robo Mwaka ya Sasa 31-Dec-20 | Robo Mwaka Iliyopita 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| I. | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji: | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (166) | (836) | (2,247) | 205 |
| | Marekebisho Kwa Ajili ya: | | | | |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (770) | 396 | 1,723 | (752) |
| | -Hasara Katika Mali za Kudumu | 113 | 113 | 444 | 110 |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji kabla ya Mabadiliko ya Mtajikazi | (822) | (327) | (80) | (437) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mikopo | (868) | (1,439) | (4,412) | 931 |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali nyingine | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (8) | 914 | 3,720 | (788) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za muda mfupi | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana Inayohitajika Kisheria | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (25) | 159 | (727) | (400) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 8 | 108 | 271 | 344 |
| | -Kodi iliyolipwa | (31) | - | (31) | - |
| | -Menginevyo | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uendeshaji | (1,746) | (585) | (1,259) | (351) |
| II. | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | Gawiwo Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (18) | (165) | (515) | (65) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Menginevyo (hamisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (18) | (165) | (515) | (65) |
| III. | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha: | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | 2,606 | (690) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (4,000) | 4,000 | (4,000) | - |
| | Madeni ya Muda Mrefu | 3,950 | 2,600 | 6,600 | 700 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawiwo Lililipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Menginevyo | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | (50) | 6,600 | 5,206 | 10 |
| IV. | Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha T | (1,814) | 5,850 | 3,432 | (405) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka | 8,968 | 3,118 | 3,710 | 4,115 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka | 7,154 | 8,968 | 7,142 | 3,710 |

[illegible]

| Jina Kamili | Sahihi | Tarehe | Jina Kamili | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|---|---|
| [illegible] | | [illegible] | [illegible] | | [illegible] |
| [illegible] | | [illegible] | [illegible] | | [illegible] |
| [illegible] | | [illegible] | | | |

## ADA NA GHARAMA ZA BENKI

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Akaunti za Akiba | |
| | Kufungua akaunti | Bure |
| | Ada ya akaunti kwa mwezi | 5,900 |
| | Taarifa ya akaunti | 3,540 |
| | Kufunga akaunti | 11,800 |
| | Kubadili kadi ya benki | 8,850 |
| | Kima cha chini kuendesha akaunti | 10,000 |
| | Kima cha chini cha Akiba na Biashara akaunti | 50,000 |
| | Kima cha chini cha akaunti Binafsi | 30,000 |
| | Ada ya Muamala | 1,700 |
| | Ada ya kutoa kwenye ATM | 1,300 |
| | Uthibitisho wa Salio kwenye ATM | 300 |
| | Taarifa fupi ya akaunti kwenye ATM | 500 |
| | Riba akaunti ya akiba (kwa mwaka) | 4.00% |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Mikopo (Tzs) | |
| | Mkopo wa Biashara | (3.00%-4.50%)/mwezi |
| | Mkopo wa Kuboresha Makazi | 3.00% /mkopo |
| | Ada ya Kuandaa Mkopo | 4.72% /mkopo |
| | Bima ya Maisha | 2.50% /mkopo |
| | Adhabu ya Kuchelewa kulipa | 0.5% kwa kila rejesho lilocheleweshwa |

## Minimum Disclosures of Bank Charges and Tariffs

TARRIFS ON ACCOUNTS

| HAKIKA SAVING ACCOUNT | | TZS ACCOUNT | USD ACCOUNT |
|---|---|---|---|
| Maintenance fee (per Month) | | TZS 2500 | Free |
| Withdrawal fee @ counter | | TZS 1,500 | 1% of the amount |
| Withdrawal fee @ UMOJA ATM | | TZS 1,300 | N/A |
| Dormant account fee (per Month) | | TZS 2500 | USD 2 |
| Annual Interest rate (%) | | 2% | 2% |
| Number of withdrawals (per month) | | 2 | |
| Minimum Amount to qualify for interest (Average per month) | | TZS 50,000 | |
| Mteja wa familia | | Free | N/A |
| BIASHARA PLUS ACCOUNT Current | | TZS ACCOUNT | USD ACCOUNT |
| Minimum Balance | | TZS 20,000 | USD 20 |
| Minimum Operating Balance | | TZS 5000 | USD 5 |
| Transaction below Minimum Operating Balance fees | | TZS 700 | USD 1 |
| Maintenance fee (per Month) | | TZS 6,000 | USD 6 |
| Withdrawal fee @ counter | | TZS 1,500 | 1% of the amount |
| Withdrawal fee @ UMOJA ATM | | TZS 1,300 | N/A |
| Counter cheque fee | | TZS 2,000 | |
| Dormant account fee (per Month) | | TZS 2500 | USD 2 |
| KIDS ACCOUNTS | | TZS ACCOUNT | |
| Minimum Opening Balance | | TZS 10,000 | |
| Maintenance fee (per Month) | | Free | |
| Withdrawal fee @ counter | | TZS 2,500 (1 free per quarter) | |
| Dormant account fee (per Month) | | TZS 2500 | |
| Closing fee | | Free | |
| Annual Interest rate (%) | | 4% | |
| Minimum Amount to qualify for interest (Average per month) | | TZS 100,000 | |
| MAVUNO ACCOUNT | | TZS ACCOUNT | |
| Withdrawal fee | | TZS 1,500 | |
| Interest Rates per year | | | |
| Balance [illegible] | | 3% | |
| Balance [illegible] | | 4% | |
| Balance [illegible] | | 5% | |
| Balance [illegible] | | 6% | |
| Balance [illegible] | | 7% | |
| Mteja wa familia | | Free | |
| Number of withdrawals (per month) | | 2 | |

TARIFFS ON LOAN PRODUCTS

| Products | Product Range | Processing fee | Insurance |
|---|---|---|---|
| [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| ME Plus [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| SME [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
| SME [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |

TARIFFS ON FINANCIAL SERVICES

| BANK TRANSFERS | | | |
|---|---|---|---|
| Done at the tills/branch | TZS | USD | |
| Transfers within Letshego (same or different clients) | Free | Free | |
| Domestic transfers (in Tanzania) | | | |
| TISS | TZS 10,000 | USD 10 | |
| Administrative fee for SWIFT | TZS 1,000 | USD 1 | |
| At UMOJA ATM | | | |
| Fund transfers (Intra bank) | TZS 300 | | |
| Fund transfers InterBank | TZS 1,300 | N/A | |
| Cardless transfers | TZS 750 | N/A | |
| M-PESA TRANSFERS | TZS | USD | |
| Tigopesa to Account from Mobile phone (deposit or loan repayment) | 1,000 | N/A | |
| M-Pesa to Account from Mobile phone (deposit or loan repayment) | 1,000 | N/A | |
| M-Pesa Normal agent | | | |
| Buy or Sell your E-Money | Vodacom tariffs | N/A | |
| M-Pesa Super Agent | | | |
| Agent buying /Selling E-Money | Free | N/A | |
| ATM UMOJA CARDS | | | |
| UMOJA card issuance fee | TZS 10,000 | | |
| Replacement card (Stolen, worn out, expiry) | TZS 5,000 | | |
| ATM Balance enquiry & statement | TZS 300 | | |
| INTERNAL CHEQUES | | | |
| Chequebook issuance fee | TZS 7,800 (25 Leaves) | USD 9 (25 Leaves) | |
| | TZS 13,400 (50 Leaves) | USD 17 (50 Leaves) | |
| | TZS 22,300 (100 Leaves) | USD 37 (100 Leaves) | |
| Withdrawal fee @ counter | TZS 1,500 | 1% of the Withdrawal amount | |
| LetsGo Mobile | TZS | | |
| Registration | FREE | | |
| Balance Enquiry & statement | TZS 300 | | |
| Airtime | Free | | |
| Bill Payments | Free | | |
| Transfer Bank to Wallet | TZS 1,300 | | |
| Transfer Wallet to bank | TZS 1,300 | | |
| Intrabank transfer | TZS 300 | | |

# DC akumbuka watoto wa mazingira magumu

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Hashim Komba, amesherehekea siku yake ya kuzaliwa kwa kutoa msaada wa vyakula na vitu mbalimbali, kwa yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Miongoni mwa vyakula hivyo ni mahindi kilo 100, mchele kilo 50, sare za shule, madaftari baiskeli, sabuni na taulo za kike, huku akiwasisitiza kusoma kwa bidii kwa ajili ya maendeleo yao ya baadaye na taifa kwa ujumla.

Komba ambaye alitoa msaada huo juzi, alisema, makundi hayo yanahitaji faraja ili yajione kuwa yako kwenye jamii inayoyajali, hivyo akatumie siku ya kuzaliwa kula nayo na kuyapa msaada huo wa vyakula na vitu vingine.

"Kuna yatima ambaye amefaulu kwenda Namatula Sekondari, lakini anaishi mbali, huyo nimempa baiskeli ili imsaidie katika usafiri, na nimewataka wote wasome kwa bidii ili baadaye wafaidika na elimu," alisema Komba.

Alifafanua kuwa, amechukua hatua ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa kwa kula pamoja na makundi hayo na kuyapa msaada, kwa kuwa hilo ni jukumu la kila mmoja.

"Ni muhimu kuwafanya yatima na wale wenye mahitaji maalum kuwa na maisha yasiyokuwa na tofauti na watu wengine, hivyo kila mmoja wetu kwa nafasi yake anatakiwa kuwasaidia," alisema.

"Tumewapa watoto wetu sare zao za shule bure kila mmoja na madaftari ya kuanzia mhula huu wa masomo.

Alisema, yatima na wenye mahitaji maalum wanahitaji kusaidiwa na kila mtu, kwa kuwa hilo ni jukumu la Watanzania wote, hivyo yeye ameamua kufanya sehemu yake, na kwamba kila itakavyowezekana, ataendelea kuwasaidia.

# Upepo waacha wananchi bila makazi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

KAYA 24 zimeachwa bila makazi katika Kijiji cha Kamsamba wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa, baada ya nyumba 24 kubomoka kutokana na upepo mkali.

Ofisa mtendaji wa kijiji hicho, Mary Mahenge alisema tukio hilo lilitokea Januari 25, majira ya jioni.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Christina Sangu, alisema siku hiyo kulikuwa na upepo ambao ulikuwa ukivuma kwa kasi kubwa kiasi kwamba wakazi karibu wote wa kijiji hicho walilazimika kuingia ndani ya nyumba zao na kujifungia.

Kadiri muda ulivyokuwa ukiongezeka ndivyo upepo huo uoivyokuwa ukiongezeka kasi, hali iliyosababisha watu kuanza kutoka nje ya nyumba zao kwa kuhofia nyumba inaweza kubomoka wakati wao wako ndani na wakajeruhiwa. Baada ya muda kidogo, walishangaa kuona angani wingu jeusi likianza kushuka chini na upepo ulikua mkali zaidi na kutokea kimbunga ambacho kilisababisha nyumba 25 kuezuliwa mapaa na baadhi kubomoka kabisa.

"Kitendo hicho kilizua hofu sana kwetu, hadi wengine tukadhani ndio mwisho wa dunia, wengine waliangua vilio, wengine wakawa wanapiga kelele wakiomba Mungu awasaidie... Yaani ilikua ni tafrani tupu kwetu, tumeachwa bila makazi tunahitaji msaada" alisema.

Siku moja baada ya tukio hilo Mtendaji wa Kata ya Miangalua, Didas Kayanda, alifika kijijini hapo akiwa na unga wa ugali kilo 120, wenye thamani ya Sh. 200,000 ukiwa ni msaada kutoka kwa Mbunge wa Kwela, Deus Sangu, ambapo kila kaya iliyopatwa na maafa hayo ilipewa kilo tano za unga huo ili ziwasaidie katika kipindi hiki kigumu.

Diwani huyo aliwataka wananchi wa kijiji hicho kupanda miti katika eneo lao kwani iwapo kutakuwa na miti ya kutosha, itasaidia kupunguza kasi ya upepo kimbunga kinapotokea, hivyo hakutakuwa na madhara makubwa kama yanayo wakumba hivi sasa.




Mkuu wa Idara ya Kidigitali na Huduma Mbadala wa Benki ya Exim, Silas Matoi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), wakati wa kutangaza washindi wa kampeni ya benki hiyo ijulikanayo kwa jina la ya 'Chanja Kijanja na Exim Mastercard' jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni maofisa waandamizi wa benki hiyo, Callist Butinga (kushoto) na Paritosh Babla. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Exim yamwaga zawadi ada za shule

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imetangaza washindi wa kampeni yake ya 'Chanja Kijanja na Exim Bank Mastercard', huku ikigawa zawadi mbalimbali kwa washindi hao.

Miongoni mwa zawadi hizo ni ada za shule na safari ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa washindi wa jumla wa kampeni hiyo.

Kampeni hiyo iliyodumu kwa mwezi mmoja, ilianza Desemba mwaka jana, ikilenga kuhamasisha wateja wake kutumia kadi za MasterCard za benki hiyo wanapofanya manunuzi au malipo ya mahitaji muhimu kwenye maduka (Shopping) pamoja na ununuzi wa bidhaa kimataifa kupitia mtandaoni.

Kati ya washindi watatu wa jumla wa kampeni hiyo jana, ilishuhudiwa washindi wawili wakichagua zawadi ya kulipwa ada ya shule pamoja na vifaa vyote vya shule kwa mtoto mmoja kwa kila mshindi. Mshindi mmoja akichagua zawadi safari ya kutembelea Hifadhi ya Taifa Serengeti akiwa na mwenza wake huku kila kitu kikiwa kimelipiwa.

"Benki ya Exim inaelewa changamoto ambazo wazazi wanakabiliwa nazo wakati wa kufungua shule. Wafanyakazi wetu wengi ni wazazi pia, kwa hivyo tunaelewa hizi changamoto. Tunaamini zawadi za namna hii zitapunguza mzigo wa kifedha kwa wazazi na walezi katika katika kipindi hiki." Alisema Mkuu wa Idara ya Kidigitali na Huduma Mbadala wa benki hiyo, Silas Matoi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye hafla hiyo iliyofanyika makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam.

Alisema kampeni hiyo imehitimishwa kwa mafanikio makubwa yaliyotokana na mwitikio mkubwa kutoka kwa wateja wa benki hiyo hatua ambayo inadhihirisha uhalisia wa huduma zinatolewa na benki hiyo kwa wateja wa benki hiyo.

"Kwa mwitikio huu tumebaini ongezeko kubwa la matumizi ya huduma zetu za kidigitali kutokana na mwenendo wa mfumo wa maisha ya wateja wetu kitu kinachotupa mrejesho muhimu utakaotusaidia kuendelea kubuni huduma bora zaidi zinazoendana na hitaji hilo la wateja wetu. Zaidi tunashukuru na kujivunia zaidi kuona kwamba wateja wetu wanafurahia huduma zetu kulingana na matarajio yao ambayo ni kupata huduma za haraka, rahisi na salama kwao," aliongeza.

Matoi alihamasisha wateja wa benki hiyo kuendelea kufurahia huduma za kidigitali hata baada ya kuisha kwa kampeni hiyo.

Kwa upande wao washindi Baraka Kimaro, Khamis Mansour na Mustafa Albaghdadi walionyesha furaha yao na shukrani baada ya kupokea habari za ushindi huo, huku wakielezea kuridhishwa zaidi na uhakika na ubora wa huduma za kibenki ikiwaamo zile za mtandaoni na kwenye matawi wanazopata kupitia taasisi hiyo.

ama
ALHAMISI JANUARI 28, 2021
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

## Uhakika maji ulivyowathibitishia wanafunzi afya, mahudhurio shule



Ukurasa 14

## Mila na umaskini zinavyochangia kuibuka kwa magonjwa ya akili

MRATIBU AFYA NA UZAZI:

# Uzazi Mpango unavyobaki fumbo gumu kwa wazazi mkoani Kigoma

• Kajifungua mara 9, anaendelea • Mimba miezi minne baada ya kujifungua • Wapo wasiotaka neno 'mpango'

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

USEMI wenye ukweli kwamba watoto ni muhimu cha familia kwa sababu inadumisha furaha na upendo kwa wanandoa. Lakini, ili furaha hiyo ipatikane ni lazima wazazi wawe na uwezo kuwalea na kuwapatia watoto mahitaji muhimu kwa ajili ya ustawi wao.

Inapoingia katika uhalisia mkasa wa mwanamama Chausiku Adamu, mkazi wa kata ya Nguruka wilayani Uvinza mkoani Kigoma, kuko tofauti. Amebahatika kupata watoto tisa, wanaompa wakati mgumu kuwahudumia.

Huenda shauku ya mama huyo kupata idadi hiyo ya watoto, ndiyo imemfikisha alipo sasa. Alijifungua mtoto wa kwanza mwaka 1997 na alipokuwa na umri miaka 24 na tangu wakati huo ndoto yake,imekuwa kuzaa watoto wengi kadri awezavyo.

Kutokana na shauku hiyo, alikuwa akipata mimba miezi minne hadi mitano kila alipojifungua mtoto, jambo lililosababisha awe na mfululizo huku watoto wake wanaopishana umri wa mwaka mmoja hadi mmoja na nusu.

Kwa sasa idadi hiyo ya watoto tisa anaiona kuwa kubwa kutokana na kushindwa kumudu gharama za kuwahudumia na kuwapatia mahitaji muhimu kama mavazi na sehemu bora ya kulala.

"Maisha yamekuwa magumu siyo kama kipindi cha nyuma, yaani wanangu wanavyoishi siyo kama ninavyotaka, watoto wanakosa hadi nguo za kuvaa na sehemu ya kulala," anasema Chausiku, mwenye umri wa miaka 38.

Wakati maisha yakiwa magumu, pia Chausiku amepitia changamoto mbalimbali za kiafya zilizosababishwa na kujifungua watoto mfululizo.

"Awali nilikuwa najifungua bila matatizo yeyote, lakini mimba ya mtoto wa tisa ilinisumbua sana, kwani nilivuja damu nyingi, hivyo nimeamua nibadili mtazamo," anasema Chausiku, anayeishi na mume wa ndoa.




Aliyekuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alipomkabidhi chandarua chenye dawa, Mwantum Mohammed, katika uzinduzi wa ugawaji wake, Mwandiga Kigoma. **PICHA: MTANDAO**

Huyo ni miongoni mwa wanawake wa mkoani Kigoma, ambao ni wazito au ha watumii njia za uzazi wa mpango, jambo linalowafanya kuzaa watoto bila ya mpangilio na kujikuta wakipata changamoto za malezi, kiuchumi na kiafya wao na watoto wao.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, uzazi wa mpango ni uamuzi ya hiari ya mtu au wenza juu ya ni wakati gani waanze kuzaa, watoto wangapi wazae, wapishane kwa umri gani na lini waache kuzaa.

Baadhi ya njia za kisasa na asili za uzazi wa mpango ambazo zinaweza kutumiwa na wanawake ili kupanga vizuri watoto ni pamoja na njia ya vichecheo, vidonge, njia ya dharura ya vidonge, kondomu na kalenda.

**HALI HALISI**

Ripoti ya Utafiti wa Afya ya mwaka 2010 (Tanzania Demographic and Health Survey (TDHS 2010)) iliyotolewa na

INAENDELEA UK.13

AFYA

MTAMA – LINDI

# Uhakika maji ulivyowathibitishia wanafunzi afya, mahudhurio shule

• Vyoo bora vimo katika mlolongo • Mradi msaada thamani mabilioni

**Na Zuwena Shame**

SHIDA ya maji inajulikana kuwapo katika shule nyingi za msingi nchini, sambamba na kukosa vyoo bora ni adha inayokabili shule nyingi, huku ikiwa sehemu ya vyanzo vya magonjwa. Wilaya ya Mtama mkoani Lindi, ni sehemu inayoguswa na hoja hiyo.

Wakati wakazi walipoguswa na wako katika hatua ya kutafuta majibu, ndipo wakaibuka wadau kuwa sehemu ya mapambano, pale wanapochimba visima na kujenga vyoo bora shuleni.

Ni msaada unaoendana na kuwafundisha njia mbalimbali za kutumiwa namna bora za kunawa mikono anaziorodhesha ziko saba, magonjwa ya kuambukiza kama vile kuhara yanapoibuka.

Ofisa Mipango ya Maji na Usafi Mazingira kutoka shirika lisilo la kiserikali la Heart to Heart Foundation lenye makao makuu Korea Kusini, (KOICA), Estoni Waliha, anasema wanalazimika kuelimisha jamii na walimu wa afya, kunusuru wanafunzi na jamii inayowazunguka, katika namna endelevu.

"Wanafunzi huwa tunawajengea uwezo kwa kupitia miongozo ya wizara kwa kutengeneza timu kwa walimu wakuu na walimu wa afya kwa kuzifahamu mbinu za kuunda klabu za afya, ili ziweze kuwa endelevu kwa kupitia walimu hao, ili programu hizo ziweze kufanyika," anasema.

Anasema, mwaka jana walifanya kazi na shule 63 katika tarafa tatu za Rondo, Mtama na Nyangamara ambapo mwaka juzi zilikuwa shule 43 na vituo vya afya 19".

"Yapo magonjwa yatokanayo na maji, namna gani ya kuyazuia pia ili kuwasiadia wamama wenye watoto chini ya miaka mitano ili kuondokana na magonjwa ya kuharisha."



Ndivyo yalivyo mabomba ya maji yanayowahudumia wanafunzi Shule ya Msingi Mtama, Lindi. **PICHA: ZUWENA SHAME**

### MRATIBU MIRADI

Mratibu wa Miradi katika shirika la Heart to Heart Foundation Abrahamu Msofe, anaeleza walivyowekeza inajumuisha ujenzi wa vyoo vinavyohitaji maji mengi, inayowalazimu kuchimba visima katika maeneo hayo.

Anasema wameshajenga vyoo 27, wakiegemea mwongozo wa serikali unaojumuisha hitaji la vyoo maalum vya walemavu na cha kike kwa ajili ya kujisitiri, mrdi unaogharimu hitaji la dola za Marekani milioni 1.5 (Sh. bilioni 3.45) unaotekelezwa kwa miaka mitatu.

> **Ukosefu wa maji ulisababisha wanafunzi wawe kero mtaani, kwakuwa walikuwa wakitembea kutafuta huduma hiyo katika maeneo mbalimbali mengine yalikuwa hatarishi kwao.**

"Kwa kweli shule nyingi za msingi hazina maji na vyoo vingi sio bora na vingine ni hatarishi kwa afya za watoto ndio maana tuliona kuwa wana uhitaji mkubwa tukaja na mradi huu ili kuondoa kero kwa wanafunzi," anasema.

### SERIKALI YA WILAYA

Mkuu wa Wilaya ya Mtama, Shaibu Ndemanga, anasema ukosefu wa maji na vyoo bora unachangia magonjwa ya mlipuko shuleni, hasa ngazi ya msingi na kuna jitihada za serikali kukabili majanga hayo.

Ili kuweka hayo sawa, Mkuu wa Wilaya anaeleza sababu yao wao kunahamasisha na kuanua kampeni majumbani wajenge vyoo bora, ili mtoto awe salama nyumbani, pia shuleni.Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama, Dunstan Ntauka, anaunga mkono mkakati huo akiamini utasaidia kuondoa tatizo kubwa la maji kwenye shule za msingi.

"Wapo wadau wengi wanaoweza kushirikiana na Heart to Heart, ili kumaliza kabisa changamoto hii kwetu...inatatuliwa sehemu tu, ila eneo kubwa bado katika maeneo mbalimbali ya wilaya yetu katika shule zetu," anasema Ntauka.

### WAHUSIKA WANENA

Seif Mavelle, Mwalimu wa Shule ya Msingi Mtama, anasema kupatikana maji shuleni, kunasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo, huku vyoo vikiwa bora zaidi.

Anarejea ulihalisia uliopo kuwa, awali hata usafi wa shule na mazingira uliishia katika kufagia tu, lakini baada kujitosheleza kwa maji, sasa wameanzisha bustani na miradi inayotumia maji, kwa kupanda maua kuzunguka shule.

Mavelle anataja manufaa mengine ni wanafunzi kupata huduma ya maji ya kunywa shuleni, hali ambayo tofauti sana na zamani. Anaendelea: "Imefikia wakati asubuhi na jioni tunamwagilia maji kwenye mimea miti na maua.

"Ukosefu wa maji ulisababisha wanafunzi wawe kero mtaani, kwakuwa walikuwa wakitembea kutafuta huduma hiyo katika maeneo mbalimbali mengine yalikuwa hatarishi kwao."

Mwalimu wa Afya na Miradi wa shule hiyo, Florah Ngowi, anasema upatikanaji maji shuleni umesaidia wanafunzi, walimu pamoja na hata baadhi kuimarisha ufugaji kuku katika jamii yao.

Akiweka faida ya kiafya iliyoko, ni kwamba wapo wanafunzi waoga shuleni, si watoro na sasa wako mbali na maradhi kichocho. Mwalimu Florah anaendelea:

"Hali ilikuwa ngumu, japo natoa taulo shuleni, lakini kufuata maji zamani kulisababisha watoto wa kike wengi kuwa watoro shuleni kutokana na kero ya maji.

"Upatikanaji maji umesaidia wanafunzi kwa kiasi kikubwa, umesaidia hata uboreshaji mazingira, pia mwonekano wa shule umekuwa wa kuvutia.

"Uwapo wa tatizo hilo (maji) umekuwa ukichangia watoto wengi kutembea umbali mrefu kufata maji, ili kufanyia usafi vyooni na mengine kuweka katika vyoo hivyo, huku wakishindwa kuweka maji ya kunawa na kumwagilia maua katika shule zao.

"Pia, upatikanaji maji umeweza kusaidia watoto wa kike kuwa wasafi kupunguza utoro hasa wakati wa hedhi, ambao ulikuwa ukiwafanya warudi majumbani huku wakikosa baadhi ya vipindi kutokana na ukosefu wa maji shuleni," anasema Ngowi.

Mwanafunzi Shule ya Msingi Mtama, Timotheo Chiwembi, anasema ukosefu wa maji uliwafanya watembee umbali mrefu kutafuta huduma, hali iliyowapitisha katika maeneo yasiyo salama.

"Wakati mwingine tulipata magonjwa mbalimbali kama vile kichocho. Hii ilitufanya baadhi ya wanafunzi kuwa watoro darasani na wengine walikosa vipindi wakati wakitafuta maji," anasema.

Chiwembi Anaendelea: "Serikali inajua ina wajibu wa kutusaidia sisi, ili tuweze kupata huduma zote muhimu."Uwapo wa maji umetupa nafasi sisi wanafunzi kuweza kupanda maua na miti.

"Tukishirikiana na Mwalimu wa Mazingira na hapo tunapeana zamu ya kumwagilia maji, lakini tunapata maji safi ya kunywa, tumetengewa jaba kubwa ambalo linakuwa na maji ya kunywa tu, pia kila kona zipo ndoo za kunawa maji. "Sio wote tulioweza kubeba ndoo kwa umbali ule, lakini tulilazimika kufanya hivyo, kwa kuwa ilikuwa lazima sisi kufuata maji mtoni ili kufanya usafi chooni na kuweka maji vyooni, hilo lilikuwa jukumu kubwa kwetu."

Mwanafunzi Arafa Ngonyoko, anasema ujenzi wa vyoo bora na upatikanaji wa maji, umewasaidia wao wasichana hasa wakati wa hedhi, akieleza:

"Kabla hatujawa na maji tulikuwa tunaenda mabondeni kutafuta maji mbali kabisa na wakati mwigine kwenye mfereji au kisimani hakukuwa na usalama wengi. Tulihofia kubakwa, pia tuliogopa mapori yalikuwa kando ya maji

"Hakuna wakati mgumu tuliokuwa nao kama sisi watoto wa kike ambapo tulilazikmika kukaa majumbani wakati wa hedhi hadi muda unaisha, ndio tunarudi. Hii ilitokana na kukosekana huduma za maji, unashindwa kunawa. Inabidi tu ukae nyumbani" anaeleza Arafa.

AFYA

## MRATIBU AFYA NA UZAZI:

# Uzazi Mpango unavyobaki fumbo gumu kwa wazazi mkoani Kigoma

**INATOKA UK.11**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaeleza asilimia 70 ya wanawake walioolewa Tanzania wanatamani kuchelewa kupata watoto au kupanga idadi ya watoto watakaowazaa.

Pia, anafafanua kuhusu ripoti hiyo kwamba, asilimia 27 tu ya wanawake ndio wanaotumia njia za kisasa za uzazi wa mpango, hali inayosababisha wanawake wengi kujifungua mapema na wana watoto wengi, hali inayojiweka dhahiri mkoani Kigoma.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Kigoma Dk Ernest Teyumwete, anasema mfumo wa taarifa za huduma za afya (Health infomation system) unaeleza hadi Novemba mwaka jana, matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango ulifika asilimia 34 katika mkoa huo.

Hata hivyo, takwimu hizo zinaonyesha ishara ya matumizi ya njia hizo yanashuka tangu mwaka 2018, kwani wakati huo yalikuwa katika asilimia 46, mwaka uliofuata 2019 yalikuwa asilimia 40, kabla hayajashuka zaidi mwaka 2020. Kiwango hicho cha matumizi ya njia za kisasa kwa wanawake wa mkoa wa Kigoma, kinaelezwa kiko chini ya kiwango kinachopendekezwa na serikali cha walau asilimia 60.

### NINI SABABU?

Kunatajwa sababu za wanawake wa mkoa huo kutokutumia njia za kisasa za uzazi wa mpango, ikiwamo zinazohusishwa na masuala ya kiimani na uelewa mdogo wa utendaji na faida za njia hizo katika kuendeleza familia bora.

Mkazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji (jina tunalo), baba wa familia ya watoto saba, anaeleza hayuko tayari kumruhusu mke wake kutumia njia za kisasa za uzazi wa mpango, kwa sababu ni kinyume na maelekezo ya imani yake.

Mtazamo huo ndi una mustayakabali, baadhi ya wanawake hawatumii mbinu hizo za kisasa za uzazi wa mpango, sababu kuu ni mitazamo hasi inayohusuasana nayo, ikiwamo.

Pia, wanalaumu kalenda kwamba kuna wakati wake unakuwa mdogo na unawafanya wazae watoto bila mpangilio sahihi.

Mkazi wa Uvinza mkoani humo, Maria (jina la pili) mwenye umri miaka 32, anasema aliwahi kutumia njia hizo, lakini baadaye aliamua kuachana nazo kwa sababu alipata mabadiliko, ikiwamo kupata hedhi mfululizo kwa mwaka mzima.



Huduma ikiendelea katika Kituo cha Afya Nguruka, wilayani Uvinza, Kigoma. Ni eneo anakopatikana mama mwenye wa watoto tisa. **PICHA: MTANADAO**

> **Madhara ya kiakili yanayosababishwa na makosa katika siku 1000 za mwanzo hayana mbadala labda Mungu mwenyewe tu aingilie kati.**




"Niliwahi kuchoma sindano moja tu ya uzazi wa mpango, lakini ilinisababishia kupata hedhi mwaka mzima na baada ya kuacha sikupata hedhi kwa mwaka mzima mfululizo," anaeleza mama huyo, mwenye watoto sita.

### MRATIBU AFYA NA UZAZI

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Kigoma Dk Ernest Teyumwete, anasema mwanamke anapaswa kupumzika angalau miaka miwili kabla ya ujauzito mwingine, ili kuimarisha mfuko wake wa uzazi.

Hiyo inamsaidia kupunguza hatari ya mfuko huo kuchanika au mwanamke kuvuja damu nyingi wakati wa kujifungua na mtoto kufariki.

"Tunasisitiza matumizi ya njia za kisasa kupanga uzazi kwa sababu ni vigumu mwanamke kufanikiwa kupanga uzazi pasipo kuzitumia, hivyo jamii inapaswa kuachana na mitazamo hasi ambayo imekuwa ikisababisha madhara ya kiafya kwa wanawake," anasema Dk. Teyumwete.

### OFISA LISHE

Ofisa Lishe Mkoa wa Kigoma, Naomi Rumenyela, anakumbusha anaeleza kuwa mtoto anatakiwa kunyonya maziwa ya mama kwa miezi sita bila kuchanganya chakula kingine ili mwili wake uweze kujitengenezea kinga imara .

Watoto wakikosa lishe bora katika siku 1,000 za mwanzo, inasababisha ugonjwa wa utapiamlo na udumavu ambao uathiri afya ya mwili na akili.

"Madhara ya kiakili yanayosababishwa na makosa katika siku 1000 za mwanzo hayana mbadala labda Mungu mwenyewe tu aingilie kati," anasema Rumenyela.

Mtaalamu huyo anawashauri wanawake wa mkoa huo kuzingatia uzazi salama, ili kuhakikisha watoto wao wanakuwa na afya bora na kukua vizuri.

Kutokana na hali hiyo, Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto, Dk. Teyumwete, anasema wanaendelea kuboresha utoaji elimu ya uzazi wa mpango maeneo ya huduma za afya na kuwatumia watoa huduma ya afya ngazi ya jamii, ambayo wamekuwa wakipita nyumba kwa nyumba.

Pia, anabainisha kuwa mkoa Kigoma, umeandaa mpango wa dharura wa kukabiliana na vifo ambapo tayari wameandika andiko litakalowahusisha wadau mbalimbali kufanikisha utoaji elimu kwa jamii.

AFYA

# Mila na umaskini zinavyochangia kuibuka kwa magonjwa ya akili

**Na Jenitha Jacob**

BAADHI ya tabia za usiri zilizojificha katika mila na utamaduni wa asili katika jamii zinachangia sehemu ya watu wake ama kuendekeza au kuzua maradhi mapya.

Ni tabia zinazojikita kwa siri. Kuna mazingira zinakomaa katika jamii zetu kiasi kwamba, mtu akienda kinyume chake au kuhoji huonekana adui, hata kutengwa. Moja ya tabia hizo ni kuvumilia taratibu maskini, magumu ya maisha, rushwa na hali nyingine zisizofaa katika nyanja za kijamii na kiuchumi. Namna ya kuvumilia huku mtu akiumia kwa siri ni staili inayopewa usemi 'kufa na tai shingoni' iko katika maeneo mengi, sababu kuu ikiwa iko katika mila na utamaduni.

Inaelezwa kwamba, uvumilivu unakuwa muhimu kwa mtu au jamii wakati wa kutafuta hatua maishani. Hata hivyo, ndani ya kanuni hiyo ya uvumilivu, ukosefu maadili daima haupewi nafasi kubwa. Mara zote inatajwa athari ya kuvumilia hata yasiyofaa kuvumiliwa, yamesababisha kuwapo magonjwa ya akili katika jamii za Kiafrika, ambayo huenda hayajulikani au hayapo wazi kwa kiwango kikubwa.

Ni jambo linaloangukia masikitiko, hata wanapogundiliwa wagonjwa waliokosa huduma mahsusi kwa sababu ya utamaduni huo wa 'uvumilivu' na 'usiri' unachangia kudumaza maendeleo.

Kutopatiwa matibabu na kutogundulika wagonjwa wa akili, kunasababisha jamii kuzama zaidi kwenye umaskini, kwani wagonjwa hawashiriki katika shughuli za kiuchumi kujiendeleza.

Pamoja na kuwa halitiliwi maanani, tatizo ni kubwa.

Mwandishi Lansana Bberie, katika makala iitwayo 'Mental illness: Invisible but devastating' katika jarida la kimataifa la African Renewal, anaonyesha ushirikina unavyohusishwa na magonjwa ya akili Afrika.

Kupitia marejeo ya takwimu, ana angalizo la kutaka hatua zichukuliwe kutokana na mikasa ya watu kujinyonga. Pia, kuna makadirio kila watu 100,000, wastani kati ya mtu mmoja na wawili hujiua. (wastani 1.4)

**KULIVYO NCHINI**

Mwaka 2014, aliyekuwa Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Donald Mbando, alisema Tanzania ilikuwa na zaidi ya wagonjwa 450,000 wenye matatizo ya afya ya akili, sehemu kubwa ni vijana wa umri kuanzia miaka 15.



Wanaohisiwa kuwa na matatizo ya afya ya akili, katika moja ya mitaa nje ya nchi. **PICHA: MTANDAO**

> **Mara zote inatajwa athari ya kuvumilia hata yasiyofaa kuvumiliwa, yamesababisha kuwapo magonjwa ya akili katika jamii za Kiafrika, ambayo huenda hayajulikani au hayapo wazi kwa kiwango kikubwa.**

Mganga Mkuu, aliiambia hadhira katika shamrashamra za kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani, kwamba matumizi ya dawa za kulevya yana mchango mkubwa katika idadi hiyo kubwa.

Hata hivyo, aliweka wazi kuwa wazee nao wamo katika kuathiriwa uwezo wa kufikiri, kuhisi, kutambua, kutenda na anashauri kila penye mwenendo au tabia tofauti dhidi ya jamii, mhusika anapaswa kufikishwa hospitalini, aanze kuhudumiwa.

**SABABU?**

Makala tajwa 'Mental illness: Invisible but devastating' ina orodha ya yanayochangia unyanyapaa kwa wagonjwa wa akili Afrika na mwandishi anaueleza umaskini humpatia mgonjwa huzuni na hofu, jambo ambalo lisipoangaliwa, humkosesha huduma za afya.

Watafiti AngerMeyer M and Dietrich S, wanasema matatizo kwa wagonjwa huwa makubwa, kutokana na mitazamo hasi na unyanyapaa dhidi ya wagonjwa wa akili. Pia, kuna watafiti Egbe C na wenzake waliopekua unyanyapaa nchini Afrika ya Kusini na kuanika walivyobaini kuwapo unyanyapaa wa aina mbili; ngazi ya jamii na binafsi.

Wakati unyanyapaa ngazi ya jamii unaelezea watu wanavyofikiri na kuwaona wagonjwa wa akili, unyanyapaa binafsi unazama katika mtu kujikataa na kujichukia, kwa sababu ya magonjwa yake ya akili.

Matokeo ya jumla yanatajwa kuwa zao la imani na mitazamo katika jamii husika, kuhusu magonjwa ya akilini wanayoshuhudia katika jamii zao.

Watafiti, Louis K and Roberts P, walitathmini mitazamo ya jamii kwa magonjwa ya akili katika mabara Afrika na Marekani Kaskazini, wakiangalia mustakabali wa umaskini unavyoleta huzuni, upweke, matatizo ya kisaikolojia na kutojikubali. Afrika, watafiti wanaeleza kuwa umaskini umewaletea athari katika ngazi za kaya, mataifa na kusababisha kudorora kwa maendeleo ya jumla.

Mwandishi Sickel A na wenzake katika makala yao iitwayo 'Mental health stigma update: A review of consequences' nao wana mtazamo wa athari ya akili, inavyomuangukia mtoto alipo,

Sickel anafafanua kwamba, mtoto anapokuwa na msongo wa mawazo na magonjwa ya akili, moja kwa moja anapatwa na shida kama ya kutopatiwa matunzo stahili na kunyanyaswa, ikiishia na umaskini wa watoto.

Pia, kuna watafiti kama Rao D na wenzake, wanaeleza umaskini wa muda mrefu huwa na kawaida ya kuathiri utendaji wa akili na hatimaye kuzua magonjwa ya kimwili na kiakili.

Hilo limechangia hoja kwamba kuna uhusiano wa umaskini wa Afika na maradhi ya akili yanayohusiana, kwani umaskini katika eneo hilo la dunia, ni sababu kubwa inayochangia magonjwa ya akili ndani ya jamii.

Katika kukabili magonjwa hayo ya akili, kunasisitizwa umuhimu wa wadau kushughulikia magonjwa ya akili na umaskini, kupitia utoaji elimu ya afya ya akili, ushauri nasaha, matibabu na sera za kupunguza umaskini.

**DALILI ZA AKILI**

i) Kihisia

· Kukosa furaha na kuhuzunika sana
· Kuwa na furaha sana kupita kiasi
· Wasiwasi au woga kupita kiasi, au zote pamoja.
· Kupunguza maongezi au kutoongea, au kinyume chake kuongea kupita kiasi
· Hasira za haraka hata kufikia kupiga wengine
· Kuwa na msongo wa mawazo
· Kujitenga pekee muda mrefu, au kupenda kuwa na watu kuliko kawaida
· Kukosa ari ya kazi au kufanya kazi nyingi kwa wakati mmoja bila kuzikamilisha
· Kutoonyesha hisia usoni, mfano furaha au huzuni.
· Kutojali usafi na mwonekano wake
· Kuhisi maisha hayana thamani na kuona bora kufa, kuliko kuishi na anaamua kujiua, au hata kuua wengine.

ii) Kimwili

· Hakuna nguvu au kuhisi nguvu za ziada.
· Kukosa usingizi au kulala kupita kiasi
· Hali au anakuwa na hamu ya kula iliyozidi.
· Hatulii sehemu moja au muda mrefu anakuwa sehemu moja bila ya kuhama.
· Maumivu mwilini kama kichwani, mabegani, mgongo na viungo na anapoenda hospitali, vipimo havionyeshi tatizo.

iii) Kiakili

· Kukosa umakini wa shughuli zake za kila siku
· Kusahau haraka au kupoteza kumbukumbu.
· Kukosa uwezo kupambanua mitazamo tofauti
· Kuhisi sauti zisizokuwapo na kuona visivyokuwapo.
· Imani ya isiyoendana na mila, imani au desturi za jamii yake, kama vile umaarufu au anajiamini ni Nabii, au anaamini kupokea taarifa za redioni au kwenye mitandao.
·Pia, anaamini kuwa na nguvu ya ziada kutoka nje ya mwili yake, inayomsababishia kutenda au kuwaza anachohisi kichwani.
· Anaamini mawazo yake yanapunguzwa au kuongezwa na watu wasiojulikana kama vile radio na televisheni vinazungumzia yeye, au vinaongea mawazo yake.
· Hana mawazo yenye mtiririko unaoeleweka.



## HABARI DODOMA

# Waagizwa kuhamia kwenye soko jipya

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WAFANYABIASHARA wa matunda na mboga waliopo stendi ya Sabasaba na kwenye maeneo yasiyo rasmi wametakiwa kuheshimu maelekezo ya Halmashauri ya Jiji hilo kwa kuhamia soko lililoko Makole.

Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa mboga na matunda wa stendi ya Sabasaba pamoja na wanaofanya biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Alisema jiji hilo limetoa maelekezo kwa wafanyabiashara hao kuhamia kwenye eneo lililotengwa la Makole, hivyo wanapaswa kuzingatia ili wasiingie kwenye mgogoro na Jiji.

Yuna alisema kuwa eneo lililotengwa kwa ajili ya mboga na matunda la soko la Makole, bado kuna nafasi ya kutosha na pia lina vigezo vinavyostahili vya kufanya biashara zao kwa uhuru na kwa misingi, taratibu na sheria zilizowekwa.

"Nataka kuwaambia ndugu zangu wafanyabiashara mnaofanya biashara katika stendi hii ya daladala ya Sabasaba hapa siyo rafiki kwenu hata kama mnajipatia ridhiki yenu, lakini hapa kuna msongamano wa daladala ni hatari kwenu nyinyi na wateja wenu mnaweza kuganyangwa hata na bidhaa zenu pia," alisema.

Aliongeza "Halmashauri ya Jiji limewatengea eneo la soko la Makole na mnatakiwa kuhamia huko na sivyo vinginevyo kwa kuwa lipo huru na mnaweza kufanya biashara zenu bila kusumbuliwa na magari kama ilivyo kwa hapa stendi ya daladala ya Sabasaba."

Alisema eneo hilo wanalong'ang'ania kulitumia kwa sasa ni hatarishi kwao na kwa wateja.

Kwa upande wao, wafanyabiashara hao walisema wapo tayari kuhamia soko la Makole, lakini kinachotakiwa ni kuimarisha miundombinu mbalimbali.

Mwanahamisi Omari alisema pamoja na eneo hilo la Makole kuwa na nafasi lakini inahitajika miundombinu iboreshwe.

"Sisi tupo tayari kuhamia katika soko la Makole na kuondoka katika soko la stendi ya daladala ya Sabasaba, lakini tunachoomba wafanyabiashara wote wa matunda, mboga, nyanya na vitunguu wote wasibaki humu ndani bali kinachotakiwa ni kuondoka kwenye hilo soko tulilopangiwa na halmashauri yetu," alisema.

# Mwendokasi kinara ajali barabarani

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

IMEELEZWA kuwa udereva wa mwendokasi ndio unaoongoza kwa ajali za barabarani nchini.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilbroad Mutafungwa, alibainisha hayo alipokuwa akifunga mafunzo ya waandishi wa habari 12 za usalama barabarani kwa mwaka 2019.

"Pamoja na kuwapo kwa sababu nyingi zinazosababisha ajali, lakini mwendokasi umeendelea kushika kasi ya juu kwa kusababisha madhara makubwa hususani vifo," alisema.

Akitoa takwimu mbalimbali za ajali kwa mwaka, kamanda huyo alisema kwa mwaka 2016 ajali zilikuwa 9,856, vifo 3,256 na majeruhi 8,958, mwaka 2020, ajali zilikuwa 1,714 na vifo 1,270 na majeruhi 2,126.

Aidha, alisema mwaka 2011 ajali zilikuwa 23,986, majeruhi 20,802, vifo 3,981, mwaka 2012, ajali zilikuwa 23,578, vifo 3,969, majeruhi 20,111, mwaka 2017 ajali zilikuwa 5,578, vifo 2,581, majeruhi 5,489.

"Mwaka 2013 ajali zilikuwa 23,842, vifo 4,002, majeruhi 20,689, mwaka 2018 ajali zilikuwa 3,732, vifo 1788, majeruhi 3,746," alisema.

Alisema mwaka 2014 ajali 14,360, vifo 3760, majeruhi 14,530, mwaka 2019 ajali zilikuwa 2,704, vifo 1,439, majeruhi 2,834, kwa mwaka 2015 ajali zilikuwa 8,337, vifo 3468, majeruhi 9,383.

Alisema ajali za barabarani ni tatizo na zimegharimu maisha ya wengi na hivyo kusababisha ulemavu wa kudumu na kupunguza nguvu kazi ya taifa.

Alisema zinahitajika juhudi zaidi ili kupunguza idadi hiyo ya ajali na barabara za Tanzania ziwe salama.

"Tunataka kufikia wakati tusiwe na vifo vinavyotokana na ajali nchini, Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa katika kusimamia sheria za usalama barabarani pamoja na juhudi kubwa hizo za usalama barabarani mtambuka," alisema.

Aliwahimiza waandishi hao kuendelea kuelimisha jamii juu ya kuondokana na ajali za barabarani.



Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalanganya, akipanda mti katika eneo la Mkonze jijini humo jana, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono kauli ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kuifanya Dodoma ya kijani. Kulia ni Mratibu Taifa wa umoja wa vikundi mbalimbali ujulikanao Kijiji Kipya, Henry Mbwambo. **PICHA: PAUL MABEJA**.

# Makundi maalum yapanda maelfu ya miti

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

UMOJA wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu (Kijiji kipya), umepanda miti 2,900 katika eneo la Mkonze jijini Dodoma ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa upandaji miti, mwenyekiti wa umoja huo Mkoa wa Dodoma, Kareb Mhawi, alisema kuwa wamepanda miti hiyo ili kusaidia Mkoa wa Dodoma kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mhawi alisema kuwa idadi hiyo ya miti waliyopanda itasaidia kutunza mazingira na kuondoa mkoa huo katika hatari ya kuwa jangwa.

"Tangu kauli hii ya Makamu wa Rais itolewe imesaidia sana watu, taasisi pamoja na mashirika mbalimbali kujitolea kupanda miti hali ambayo imesaidia mkoa kuondokana na hatari ya kuwa jangwa," alisema Mhawi.

Aidha, alisema kuwa pamoja na kuondoa mkoa katika hali ya jangwa pia upandaji miti umesaidia kuongezeka kwa kiwango cha mvua tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

"Hivi sasa Mkoa wa Dodoma umekuwa na mvua kubwa sana tofauti na kipindi cha nyuma hii inatokana na watu kupanda miti kwa wingi hali ambayo inasaidia hata watu kuvuna mazao ya kutosha katika kila msimu wa kilimo," alieleza Mhawi.

Mratibu wa Umoja huo Taifa, Henry Mbwambo, alisema kuwa upandaji miti huo ni muhimu katika maisha ya viumbe mbalimbali.

"Leo sisi kutoka makao makuu ya umoja huu Dar es Salaam tumeunga na wenzetu wa Dodoma kuunga mkono kauli ya Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, kupanda miti ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani," alifafanua Mbwambo.

Mmoja wa wajumbe wa umoja huo, Husna Mwichumu, alisema kuwa akiwa kama mwenyeji wa mkoa wa Dodoma ameona utofauti mkubwa na miaka ya nyuma hasa katika upatikanaji wa mvua za kutosha katika msimu wa kilimo.

"Upandaji miti unafaida nyingi sana hasa katika kutunza mazingira, kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na ukame, lakini kumesaidia kuongeza kiwango cha mvua za kutosha na kuongeza kiwango cha mavuno," alisema.

Hata hivyo, aliiomba serikali kupunguza bei ya nishati mbadala kama vile gesi, mafuta ya taa pamoja na umeme ili watu wawe na uwezo wa kutumia ili kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni yanayochangia ukataji wa miti ovyo.

# Mhudumu wa afya mbaroni kwa tuhuma za wizi wa hospitalini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, inamshikilia mhudumu wa afya wa Hospitali ya Wilaya ya Kyela, Hilda Nsasu, kwa tuhuma za kukutwa na dawa za hospitali hiyo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema jana kuwa maofisa wa taasisi hiyo Wilaya ya Kyela walipata taarifa za siri kutoka kwa wagonjwa mbalimbali waliokuwa wanakwenda hospitalini hapo kutibiwa, wakimtuhumu mtumishi huyo kuwa alikuwa anaomba na kupokea rushwa.

Alisema baada ya malalamiko kuzidi, waliamua kumwita Nsasu kwenye ofisi za TAKUKURU kwa ajili ya kumhoji ndipo walipobaini kuwa alikuwa anaiba dawa za hospitali.

Matechi alisema wakati maofisa hao wanamhoji, aliingiwa na wasiwasi hali ambayo iliwafanya waamue kumpekua kwenye mkoba wake na kumkuta amehifadhi dawa mbalimbali za hospitali bila maelezo yoyote.

Kutokana na kumkuta na dawa hizo, alisema maofisa wa taasisi hiyo waliamua kwenda kumpekua nyumbani kwake wakishirikiana na viongozi wa hospitali ndipo wakakuta amehifadhi aina mbalimbali za dawa na vifaa tiba vya hospitali hiyo.

"Kwenye mahojiano yetu na Nsasu, alikiri kuiba dawa hizo na kwamba ilikuwa kawaida yake kufanya hivyo. Kwa sasa tunaendelea na uchunguzi na tuko hatua za mwisho kuukamilisha ili afikishwe mahakamani," alisema Matechi.

Pia Matechi alisema wanaendelea kufuatilia mtandao wa wizi wa dawa katika hospitali hiyo kwa maelezo kuwa wamebaini vitu vingine ambavyo si vya kawaida kwenye uchunguzi wa tukio hilo.

Alisema kwenye uchunguzi wao walibaini baadhi ya watumishi wa hospitali hiyo, wakiwamo madaktari ambao si waaminifu ambao wanatumia fomu za Bima ya Afya za wagonjwa waliowahi kwenda kutibiwa hospitalini hapo kuiba dawa.

"Wanachukua namba za wagonjwa wa bima, wanazijaza kwenye fomu na wanaenda kwenye duka la dawa la hospitali na wanaangalia namna ya kuzitoa nje na moja ya njia wanazotumia ni hiyo ya kuwatumia wahudumu wa afya," alisema Matechi.



Wanafunzi wa chekechea katika Shule ya Msingi Uhuru iliyopo katika Kata ya Mwakibete katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wakinywa uji shuleni hapo jana asubuhi, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya Serikali kuimarisha elimu. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

# Wasambazaji gesi waonywa udanganyifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WASAMBAZAJI wa mitungi ya gesi, wametakiwa kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia biashara hiyo ikiwamo matumizi ya mizani wanapowauzia wateja ili kuepuka udanganyifu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Muhiba Chakupewa, wakati wa mafunzo kwa wajasiriamali yaliyokuwa na lengo la kuwajengea uwezo juu ya matumizi ya gesi.

Alisema ni lazima kila msambazaji wa gesi kuwa na mizani na kuipima kabla ya kuwauzia wateja kwa madai kuwa itasaidia kujua ujazo unaotakiwa kulingana na bei iliyopo.

Chakupewa alisema Sheria ya EWURA inaelekeza kuwa mbali na kumtaka msambazaji wa nishati hiyo kuwa na mizani katika eneo lake la biashara, pia ni kosa kubadilisha gesi ya mtungi wa kampuni tofauti na ile anakofanyia kazi kwa sababu kunaweza kutokea mlipuko.

"Tumebaini kuna ukiukwaji mkubwa wa makubaliano baina yetu na wasambazaji wa mitungi ya gesi za majumbani. Sheria inamtaka msambazaji kutumia mizani wakati wa kupima lakini hilo halifanyiki. Tutaanza kufanya msako wa duka kwa duka kuangalia utekelezaji wa suala hilo," alisema.

Naye Mhandisi wa EWURA, Raphael Nyamamu, aliwasisitiza watumiaji wa gesi za majumbani kuwa makini na matumizi ya nishati hiyo kwa kuhakikisha kabla ya kuanza kutumia sharti mtungi ukae dakika kuanzia 15 hadi 30 kwa ajili ya usalama wa mtumiaji.

Alisema ni vyema kabla ya kuanza kutumia mtungi unapaswa kutulia kwa muda ulioelekezwa sambamba na mtumiaji kuhakikisha umefunikwa vizuri ili kuepusha kutoa hewa au kuvuja.

Nyamamu aliwashauri wananchi kuwa makini na matumizi ya gesi ya majumbani ikiwamo kutoa taarifa kwa EWURA pindi wanapobaini mtungi umevuja au una tatizo ili kulinda usalama wao.

Pia aliwataka wasambazaji na wauzaji wa mitungi ya gesi kuzingatia kanuni, sheria, viwango na taratibu zinazotakiwa katika kulinda afya na usalama wa watumiaji ili kuepusha madhara.

Awali, mmoja wa wajasiriamali walioshiriki mafunzo hayo, Hamida Ramadhani, alihoji kuna tatizo la kutofautiana namba zinazokaa juu ya mtungi wa gesi kwa madai kuwa wanaibiwa, hivyo kuomba EWURA kuingilia kati.

Mhandisi Nyamamu, alitoa ufafanuzi kuwa sharti mtungi wowote unaopimwa ufike kilogramu 15 bila kujali namba zilizoandikwa juu ya mtungi ambao wengi hudhani ndio ujazo halisi uliopo.

# Wakumbushwa kukatia bima vyombo vya moto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAMILIKI na madereva wa vyombo vya moto mkoani Mbeya, wameshauriwa kuvikatia bima vyombo vyao ili kuwa na uhakika wa kurejeshewa mali hizo zinapoharibika wakati majanga yanapotokea ikiwamo ajali.

Mkurugenzi wa Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Asha Mohammed, alitoa ushauri jana wakati akizungumza na wajasiriamali wa Mamlaka ya Mji wa Mbalizi iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Mohammed alisema wamiliki na madereva hususani wa bodaboda wanapaswa kukata bima ili kuwa na uhakika wa maisha au mali wanapopata majanga aidha ya moto au ajali.

Pia alisema bima hiyo inatoa huduma hata kwa abiria au mtembea kwa miguu ambaye atapata madhara ya majanga hayo ili kupata matibabu au fidia kupitia chombo cha moto ambacho kilikatiwa bima.

"Baadhi ya waendesha bodaboda hawajakata bima za vyombo vyao vya moto na hii itawasaidia kuwa salama wakati wa ajali za barabarani au moto. Nawahamasisha mkate bima ili muwe na uhakika wa maisha lakini kulipwa fidia lakini mtambue kuwa bima hii ipo kwa ajili ya kumrudisha mhanga pale alipokuwa na si kumnufaisha," alisema Mohammed.

Aidha, aliwaomba wajasiriamali wa bidhaa mbalimbali kukata bima kwa ajili ya biashara zao ili wanapopata matatizo waweze kurudishiwa fidia za mali zao na kurejea upya kwenye biashara na kujikwamua na umasikini.

Alitoa fursa kwa wajasiriamali kutuma maombi kwa Shirika la Bima la ZIC kuwa wakala wa bima hiyo, ili kusogeza huduma karibu na wananchi pamoja na kujiongezea kipato.

Ofisa Bima ya ZIC, Farhat Hafidh, alisema miongoni mwa faida za kukata bima ni kumsaidia mnufaika kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha sambamba na kumpa amani ya maisha kwani yakitokea majanga mhanga atarudishiwa mali zake.

Mkurugenzi wa Shirika la Lightness Tanzania Organization, Aliko Brown, alisema baadhi ya wajasiriamali hawana uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa bima za vyombo vya moto na biashara.



# Dk. Mwinyi aipongeza JWTZ ulinzi wa nchi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amelipongeza Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kwa kazi kubwa ya kuimarisha amani na kuilinda mipaka ya nchi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Majeshi (CDF), Jenerali Venance Mabeyo, aliyefika Ikulu jijini Zanzibar kwa ajili ya kumpongeza.

Katika maelezo yake, Dk. Mwinyi alisema kuwa JWTZ, imeendelea kufanya kazi kubwa ya kulinda amani nchini na kutoa pongezi maalum kwa kuisimamia amani hiyo hasa katika kipindi cha uchaguzi mkuu uliopita.

Alisema wananchi wa Tanzania wanajivunia hatua ya jeshi lao katika kuhakikisha wanakuwa salama wao pamoja na mali zao wakati wote na kumhakikishia Jenerali Mabeyo kwamba Zanzibar iko salama.

Rais Mwinyi alisema kutokana na kuwapo kwa ulinzi na usalama, kumesababisha wananchi wa Zanzibar kuendelea kufanya shughuli zao za kujiletea maendeleo kwa amani.

Alisisitiza kwamba Zanzibar iko salama kwa vile JWTZ iko imara hatua hiyo imesababisha kuimarika zaidi.

Aidha, Dk. Mwinyi alieleza haja kwa JWTZ kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kushirikiana na vikosi vya ulinzi vya Zanzibar likiwamo Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) katika uzalishaji mali kama vile kilimo.

Alisema kwa vile shughuli zao zinakwenda sambamba kuwapo kwa ushirikiano, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji mali katika sekta ya kilimo Zanzibar hasa ikizingatiwa kwamba JKT ina uzoefu mkubwa katika shughuli hizo.

Dk. Mwinyi aliongeza kuwa licha ya juhudi zinazofanyika katika uzalishaji mali, imeonekana bado uzalishaji ni mdogo, hivyo ushirikiano huo utasaidia kufikia lengo lililokusudiwa.

Sambamba na hayo, Dk. Mwinyi alimpongez Jenerali Mabeyo na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendelea kuilinda amani na utulivu nchini pamoja na kuilinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Mwinyi pia alitumia fursa hiyo kutoa pole kwa jeshi hilo kutokana na kifo cha Brigedia Jeneral (mstaafu) Emmanuel Maganga, aliyefariki dunia katika Hospitali ya Mirambo, Tabora alipokuwa akipata matibabu. Brigedia Jeneral Maganga aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, alifariki dunia usiku wa kuamkia Januari 22, mwaka huu.

Naye Jenerali Mabeyo alitumia fursa hiyo kumpongeza Dk. Mwinyi kwa kushinda nafasi ya urais wa Zanzibar na kueleza imani ya jeshi hilo kutokana na utendaji wake wa kazi.

Jenerali Mabeyo alisema kutokana na kumfahamu na kuutambua utendaji wa kazi wa Dk. Mwinyi kwa vile aliwahi kufanya kazi naye, ana matumaini makubwa ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Pia alipongeza hatua na busara kubwa zilizotumika katika kuleta maridhiano hali ambayo itazidisha maelewano sanjari na kudumisha amani na umoja nchini.

Jenerali Mabeyo alitumia fursa hiyo, kutoa pongezi kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuendeleza amani, umoja na mshikamano walionao.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akimsikiliza Askofu wa Kanisa la Anglikana Mkunazini Jijini Zanzibar, Michael Hafidh, alipofika Ikulu kwa mazungumzo yaliofanyika katika ukumbi huo juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Watishwa mzigo matunzo ya wazee

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema watendaji wa taasisi za ustawi wa jamii wana jukumu kubwa la kusimamia matunzo ya wazee wa Nyumba za Welezo na Sebleni ikiwa ni utekelezaji wa dhima iliyoshiba ucha Mungu utakaowapatia malipo mengine makubwa ya hapo baadaye.

Hemed alisema hayo wakati akizungumza na viongozi, wafanyakazi na wazee wanaohifadhiwa katika Nyumba za Sebleni na Welezo, alipofanya ziara maalum katika mikutano miwili tofauti kuangalia mazingira halisi ya makazi ya wazee hao pamoja na kufahamu changamoto zinazowakabili. Alisema pale zinapoibuka changamoto, matatizo na hata kasoro ndogo ndogo ni vyema kwa watendaji hao kwa kushirikiana na viongozi wao, waziwasilishe katika ngazi husika bila kuvunjika moyo ili malengo ya serikali ya kuwapatia huduma za makazi ya wazee wasiojiweza yalete mafanikio makubwa.

Hemed alitahadharisha kwamba hakuna hata mzee mmoja anayeweza kulalamika bila kuwa na sababu yoyote, hivyo kinachohitajika katika mazingira hayo ni kuona busara zaidi zinatumika katika kuwapatia huduma wazee hao ili waendelee kuishi kwa amani na upendo.

Alibainisha kwamba wazee lazima wahudumiwe ipasavyo kutokana na hali halisi ya mazingira yao kiumri na afya zao ambazo hazistahili hata kidogo kukaa na njaa muda mrefu.

Makamu wa Pili wa Rais aliutaka uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuandaa utaratibu maalum wa kila mwezi utakaowapatia huduma za afya wazee hao.

Hemed alisema haipendezi na ni jambo la kusikitisha kuona mzee mwenye umri mkubwa analazimika kupanga mstari wakati anapohitaji huduma za afya hospitalini.

## Chuo chatakiwa kuboresha mitaala

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Chuo cha Utumishi wa Umma Zanzibar umetakiwa kusimamia ipasavyo mitaala ya kufundishia katika mwelekeo wa kuzalisha wanafunzi mahiri watakaokijengea sifa chuo hicho kiwe miongoni mwa vyuo vyenye hadhi ya kitaifa na kimataifa.

Makamu wa Pili Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, katika mahafali ya 13 ya Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar. Hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Tunguu Mkoa Kusini Unguja.

Wahitimu 664 walitunukiwa astashahada, stashahada na shahada katika fani mbalimbali zinazofundishwa kwenye chuo hicho.

Alisema Chuo cha Utawala wa Umma ni taasisi inayotegemewa na serikali na hata jumuiya za kiraia katika kuwaandaa wafanyakazi watakaoivusha Zanzibar kutoka kwenye uchumi wa daraja la tatu chini hadi daraja la tatu juu.

Hemed alisema taifa lina shauku ya kuona chuo kinatoa watumishi wa umma walioshiba nidhamu, heshima, uadilifu na uaminifu utakaozaa sifa zitakazowashawishi wananchi kuiamini serikali kutokana na utumishi uliotukuka wa watumishi hao.

Alisema Rais wa Zanzibar alielezea faraja yake kusikia kuwa chuo hicho kupitia wizara yenye dhamana kuwa kikao katika hatua ya kutia saini hati ya makubaliano na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwa nia ya kuwaendeleza wakufunzi na watumishi wengine katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu.

Alisema kwa vile makubaliano hayo yanatarajiwa kufikiwa katika hatua ya utekelezaji muda wowote, maandalizi yatakapokamilika ni jambo jema na linastahili kuungwa mkono kutakokifanya chuo kuwa bora zaidi kitaifa, kikanda na kimataifa.

Aliupongeza Uongozi wa Baraza la Chuo kwa usimamizi mzuri wa sera, sheria na utekelezaji wa miongozo tofauti inayotolewa katika uendeshaji wa chuo unaotarajiwa kuleta mabadiliko makubwa chuoni hapo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 5 LA 2017**
**VIOLETH J. MKOMWA MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MICHAEL MROPE WADAIWA**
**KELVIN MROPE**
**WITO KUITWA SHAURINI**

**MICHAEL MROPE**
**KELVIN MROPE**

POPOTE MLIPO VIOLETH J. MKOMWA NA WENZAKE wamefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na nyumba lililopo kinondoni (mwananyamala) shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 29/1/2021 saa TATU asubuhi mbele ya Mh MWAKIBUJA . hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo billa kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa baraza hili leo tarehe 13 mwezi wa 1 mwaka 2020.

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 25/02/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA ALPHARD NYEUSI T 363 DRV MALI YA EDWARD MAKALA, MAENEO YA NYERERE SQUAR BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No29/2021**

Ombi la CHARLES DEODATUS MFUGALE,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu VERIAN JOHN MFUGALE.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/02/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 26/01/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAU SIRI KESSY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 193 CLM.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: MBE/MBE/RB/27220/2021.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.... 2020**
**In the matter of the Estate of the LATE HUBERT PETER KAVISHE of Dodoma Municipality/ city**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PETRONILA PETER KAVISHE**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before **10 Day of 2021.**

Dated at Dodoma this 21 Day of 01 2021




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Marais Biden, Putin wajadili uhusiano wa nchi zao

**Washington,** MAREKANI

RAIS Joe Biden na Vladimir Putin wa Urusi wamezungumza kwa njia ya simu jana, kujadili masuala kadhaa ikiwamo mkataba wa kudhibiti silaha na kuwekwa kizuizini kwa Alexei Navalny.

Kulingana na Ikulu ya Marekani, wakati wa mazungumzo hayo Rais Biden, alimweleza Putin juu ya wasiwasi alionao kuhusu kukamatwa kwa mkosoaji mkubwa wa serikali ya Urusi Alexei Navalny, tuhuma kuwa Moscow ilihusika na shambulizi la mtandao la hivi karibuni dhidi ya Marekani na madai kwamba Urusi imewalipa wanamgambo kuwaua wanajeshi wa Marekani nchini Afghanistan.

**Kwa upande wa Ikulu ya Kremlin yenyewe taarifa yake imejikita kuzungumzia majibu ya Putin kwa pendekezo la Biden la kurefusha mkataba wa New START.**

Kwa upande wa Ikulu ya Kremlin yenyewe taarifa yake imejikita kuzungumzia majibu ya Putin kwa pendekezo la Biden la kurefusha mkataba kati ya Marekani na Urusi wa kudhibiti silaha nzito unaofahamika kama New START.

Ijapokuwa taarifa kutoka Washington na Moscow zimetilia uzito mambo tofauti, pande zote lakini zimeashiria kwamba uhusiano kati ya Urusi na Marekani walau katika siku za mwanzo za utawala wa Biden yataongozwa na shauku ya kutochochea mivutano, lakini vilevile bila ya kuharakisha kumaliza tofauti zilizopo baina ya mataifa hayo hasimu tangu enzi ya vita baridi.

Kuhusu suala la mkataba wa New START, marais hao wawili wamekubaliana wajumbe wa kila upande wakamilishe haraka makubaliano ya kurefusha kwa miaka mitano utekelezaji wa mkataba huo wakati muda wa sasa utakapofikia mwisho mnamo mwezi unaokuja. **DW**



Rais wa Marekani, Joe Biden na Rais wa Urusi, Vladimir Putin, walizungumza kwa njia ya simu jana, kujadili masuala kadhaa ikiwamo mkataba wa kudhibiti silaha na kuwekwa kizuizini kwa Alexei Navalny. **PICHA/DW**

## Mamia wasubiri kuondolewa kwenye kimbunga

**Buzi,** MSUMBIJI

MAMIA ya wakazi wa wilaya ya Buzi nchini Msumbiji, wanasubiri kuondolewa katika eneo la kituo cha Guara Guara baada ya nyumba zao kuharibiwa na kimbunga Eloise.

Baadhi ya wakazi waliozungumza na gazeti la nchini humo Noticias wamesema kuwa wamekuwa kwenye msururu siku ya tatu leo.

Taasisi ya kitaifa inayoshughulikia udhibiti wa majanga (INGD) ilisema operesheni zimekuwa zikiendelea kwa namna ya kuhakikisha usalama wa kila mmoja.

Baadhi ya wale walioondolewa wamepelekwa kwenye makazi binafsi huku wengine wakipelekwa kwenye vituo vya makazi.

Mkuu wa Shirika la INGD, Luisa Meque, alisema watu walipaswa kuondoka kutoka kwenye maeneo hatari mapema, Noticias imeripoti.

INGD ilisema watu wengi walipuuza tahadhari na wale walioondolewa kwanza walikwenda kituo cha Guara Guara kwa nguvu. Noticias imeripoti.

Familia nyingi zimeendelea kuwasili Guara Guara, na haijulikani itawachukua muda gani kuondolewa. **BBC**

## Virusi vya corona sasa vifo zaidi ya milioni mbili

**Washington,** MAREKANI

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na virusi vya corona, duniani imezidi 2,151,801.

Idadi ya kesi za maambukizi imezidi 100,362,000, na idadi ya wagonjwa waliopona ni 72,414,000.

Idadi ya vifo vya corona nchini India imeongezeka na kufikia 153,624. Idadi ya kesi za maambukizi imeongezeka na kufikia 10,677,000.

Idadi ya vifo katika nchi ya Urusi imeripotiwa kuongezeka kwa 564 ndani ya siku moja na kufikia 70,482. Idadi ya kesi za maambukizi nayo imeongezeka kwa 18,241 na kufikia 3,756,000.

Idadi ya vifo vya Covid-19 ndani ya siku moja nchini Iran imeongezeka kwa 79 na kufikia 57,560. Idadi ya kesi za maambukizi ndani ya saa 24 imeongezeka kwa 6,420 na kufikia 1,385,000.

Watu 4,498 wamefariki nchini Israel kwa Covid-19 hadi kufikia sasa. Idadi ya kesi za maambukizi nchini humo imefikia 606,365. Watu 20 kati ya 128,000 waliopewa dozi ya pili ya chanjo ya Pfizer na BioNTech wameambukizwa virusi. **TRT**

## Somalia yaweka masharti uagizwaji wa mirungi

**Mogadishu,** SOMALIA

WAZIRI wa Fedha nchini Somalia, Abdirahman Duale Beyle, ameondoa marufuku ya uagizwaji wa mirungi kutoka Ethiopia.

Taarifa hiyo ilisema kwamba masharti kadhaa yamewekwa ili kuuwezesha mmea huo kukubalika kuingia katika ardhi ya Somalia.

Serikali ya Shirikisho ya Somalia ilikuwa imeondoa rasmi marufuku ya uagizwaji wa mirungi (miraa) kutoka Kenya kulingana na Gazeti la the East African.

Waziri huyo, aliwaambia waandishi wa habari kuwa wafanyabiashara sasa wataruhusiwa kuingiza miraa ndani ya Somalia, lakini biashara hiyo lazima ifuate taratibu zinazofaa.

“Wafanyabiashara lazima waingize mirungi ndani ya nchi kwa njia iliyo halali kisheria,” alisema Dk. Beileh.

Mirungi ni mmea unaotumiwa kama kiburudisho cha akili, na hutafunwa sana nchini Somalia na Kenya husasan miongoni mwa jamii za Wasomali wanapobarizi kujiburudisha.

Somalia ilisitisha uagizwaji wa miraa wakati safari za ndege za kimataifa zilipositishwa mwaka jana kutokana na hofu ya maambukizi ya Covid-19. **BBC**

## Usalama waimarishwa Delhi kudhibiti wakulima

**New Delhi,** INDIA

POLISI nchini India, wameweka usalama mkali na kufunga barabara kuu ndani ya mji wa New Delhi, siku moja tu baada ya wakulima kuzusha vurugu katika mji mkuu na kusababisha kifo cha mmoja na wengine kadhaa kujeruhiwa.

Vurugu hizo ziliashiria kilele cha mzozo kati ya serikali na maelfu ya wakulima ambao wamekuwa wakipiga kambi viungani mwa mji huo tangu mwisho wa mwezi Novemba.

Wakulima hao ambao wengi wanatoka majimbo ya kaskazini mwa India likiwamo Jimbo la Punjab, wanataka mageuzi mapya katika sekta ya kilimo yafutwe, wakihofia yatawaacha kuhangaika mikononi mwa mashirika makubwa.

Juzi, wakati wa gwaride la kila mwaka la kitaifa, misafara ya matrekta ya wakulima ilivunja vizuizi vilivyowekwa barabarani kisha wakulima wakaingia katikati ya mji, hatua iliyosababisha makabiliano kati yao na polisi waliotumia marungu na kemikali za kutoa machozi. **DW**

# SILVA ATAKA KUMFIKIA RONALDO



**LONDON,** England

FABIO Silva ameeleza hamu yake ya kufikia kiwango cha Cristiano Ronaldo siku moja, kauli hiyo akiitoa wakati akizungumzia pia changamoto ya kuchukua nafasi ya Raul Jimenez kwenye timu ya Wolves.

Silva alikuwa na usajili ghali zaidi katika historia ya Wolves alipomaliza uhamisho wa pauni milioni 36 kwenda pale kwenye dimba la Molineux akitokea Porto, Septemba.

Kijana huyo mwenye umri wa miaka 18, amesaini mkataba wa miaka mitano na Wolves, na tayari amejithibitisha kama mshiriki muhimu wa kikosi cha Nuno Espirito Santo katika nusu ya kwanza ya kampeni ya msimu wa 2020-21.

Silva amefunga mabao manne katika mechi 18 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo hadi sasa, pamoja na juhudi nzuri zake kibinafsi wakati wakifungwa 3-2 dhidi ya West Brom mara ya mwisho.

Kukua kwa Silva kwa miaka kadhaa iliyopita kumemwona akilinganishwa na nahodha wa Ureno, Ronaldo, ambaye alianza kazi yake katika klabu ya Sporting CP kabla ya kwenda kucheza Manchester United, Real Madrid na Juventus.

# Fernandes: Sihitaji kupumzishwa

**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI aliyeiongoza Klabu ya Manchester United kushinda raundi ya nne ya Kombe la FA, Bruno Fernandes, amepinga madai kwamba anahitaji kupumzika.

Ni chini ya miezi 12 tangu Fernandes kujiunga na United kutoka klabu ya Sporting Lisbon na uhamisho wake wa dau la pauni milioni 47 na umeibadilisha timu hiyo.

Kutoka katika timu ambayo ilikuwa ikitaabika kufuzu katika Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, United sasa ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

"Kuchoka? Nikiwa na umri wa miaka 26, siwezi kuchoka," alisema Fernandes.

"Iwapo nimechoka, ninapofikia umri wa miaka 30 au 32, sitoweza kucheza ama nitacheza mechi moja kati ya tano. Hapana."

United iliishinda Liverpool katika Kombe la FA kutokana na mpira wa adhabu uliopigwa na Fernandes katika dakika za mwisho Jumapili iliyopita.

Baada ya kushinda mara nne, mchezaji bora wa mwezi katika ligi hiyo, kati ya mara saba, Fernandes alianzishwa kama mchezaji wa ziada dhidi ya Liverpool.





# Tuchel aanza kazi

**LONDO,** England

RASMI Klabu ya Chelsea imemtambulisha, Thomas Tuchel, kuwa mrithi wa mikoba ya Frank Lampard ambaye ametimuliwa ndani ya kikosi hicho kutokana na mwendo mbovu.

Kocha huyo ameanza kazi rasmi ndani ya Stamford Bridge kwa ajili ya kuwanoa wachezaji ambao walikuwa chini ya Lampard.

Lampard alifutwa kazi Januari 25 kabla hajapewa mkataba wa kuwa kocha mkuu ndani ya timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England na aliiacha ikiwa nafasi ya tisa ikiwa na pointi 29.

Tuchel amejiunga na Chelsea akiwa huru baada ya kufutwa kazi ndani ya Klabu ya PSG inayoshiriki Ligue 1 ambayo kwa sasa ipo chini ya Mauricio Pochettino aliyefutwa kazi ndani ya Tottenham Hotspur.

Kocha huyo amesaini dili la mwaka mmoja na nusu na una kipengele cha kuongeza mwaka mmoja mbele ikiwa atafanya kazi kwa umakini na kuipa matokeo timu yake.

Tuchel amesema kuwa anafurahi kupata kazi ndani ya kikosi hicho huku akiahidi kuonyesha ushirikiano kwa wafanyakazi wote.

# Conte: Eriksen atabaki Inter

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amebainisha kwamba, Christian Eriksen, anaweza kubaki hapo Inter baada ya kufunga bao la ushindi kwenye mchezo wa dabi ya Jiji la Milan, akisema kiungo huyo anapendwa klabuni hapo.

Eriksen alifunga bao kwa shuti kali akiwa umbali wa yadi 25 katika dakika ya 97 na kuiwezesha Inter kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Milan kwenye robo fainali ya Coppa Italia, Jumanne.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka baada ya kuanza katika mechi nne tu za Serie A msimu huu, lakini Conte alisema Eriksen alikuwa anahitajika Inter.

"Nina uhakika (bao) limempa nguvu (Eriksen) na kwa upande wetu sisi. Nilimwambia akipata nafasi apige mashuti na ndivyo alivyofanya," alisema kocha huyo wa Inter akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni kijana mzuri. Kila mmoja anampenda, tunampenda. ameinyanyua timu. Lakini ana aibu.

"Natumaini bao hili litampa ujasiri kwa sababu tunamhitaji yeye. Tunahitaji kila mtu kwenye hali hii. Nina furaha sana juu yake na ninafuraha kwa sababu tumefuzu."

Katika mchezo huo, Zlatan Ibrahimovic alifunga bao la ufunguzi, kabla ya Romelu Lukaku kusawazisha.



# LINGARD KUTUA WEST HAM



**LONDON,** England

KOCHA wa West Ham, David Moyes, anaongoza na kikosi chake katika mbio za kuwania saini ya kiungo mshambuliaji wa Manchester United, Jesse Lingard, ambaye amepoteza nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Ole Gunnar Solskjaer.

Lingard mwenye umri wa miaka 28, ameshindwa kumshawishi kocha wake Solskjaer na kupata nafasi ya kucheza kama ambavyo ilikuwa awali.

Kuna tetesi nyingi zinazomhusisha nyota huyo, lakini 'Wagonga Nyundo' wa London, West Ham wamekuwa karibu zaidi kushinda katika mbio za uhitaji wa nyota huyo.

Endapo atasajiliwa kwa mkopo, basi mchezaji mmojawapo kati ya Craig Dawson na Said Benrahma inatakiwa ajiunge nao kwa mkataba rasmi.

Moyes anamhitaji Lingard pengine kwa sababu alifanya kazi naye kipindi anakinoa kikosi cha Man United mwaka 2013.

# *Alaba agonganisha klabu kubwa Ulaya*

**MADRID,** Hispania

MPAMBANO wa kuwania kumsajili David Alaba linaendelea miongoni mwa klabu kubwa barani Ulaya.

Alaba mwenye umri wa miaka 28, anapanga kuondoka Bayern Munich mwishoni mwa msimu na iliripotiwa mwezi huu kwamba, mlinzi huyo ameshafikia makubaliano na Real Madrid.

Lakini mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria bado zinaendelea.

Real Madrid imetoa ofa kwa Alaba ya euro milioni 11 kama mshahara wake kwa mwaka na Manchester City wanajiandaa kutoa ofa ya euro milioni 14, kwa mujibu wa gazeti la AS.

Ripoti imesema kwamba, Manchester United, Liverpool, Paris Saint-Germain na Chelsea pia zinawania kumsajili Alaba.

Alaba ameshinda mataji tisa Bundesliga na mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Bayern.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA ATAREJEA LYON, ASEMA WAKALA

**●●● Je, Karim atarudi Lyon? Ndio, kwa kweli nadhani atarudi, anazungumza nami kila...**

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Real Madrid, Karim Benzema, atarejea kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, katika klabu ya Lyon, kwa mujibu wa wakala wake, Karim Djaziri.

Benzema alipitia katika akademi ya Lyon na alikaa miaka mitano na timu ya wakubwa hadi alipojiunga na Madrid mwaka 2009, kutokana na kujiimarisha kama mmoja wa wachezaji wachanga wa Ulaya baada ya kushinda mataji manne mfululizo ya Ligue 1.

Tangu ahamie Madrid, Benzema ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na mataji matatu ya LaLiga.

**Lakini Djaziri alidokeza juu ya kurudi kwenye klabu yake ya utotoni ya Lyon kwa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 33.**

“Je, Karim Benzema atarudi Lyon? Ndio, kwa kweli nadhani atarudi,” Djaziri aliiambia Inside Gones.

“Anazungumza nami kila wakati na anaangalia mechi zote za timu.

“Juu ya hayo, hajawahi kwenda kwenye Uwanja wa Groupama na akilini mwake ni kitu anachotaka, ana Lyon moyoni mwake.”

Benzema amefunga mabao 10 ya LaLiga kwa mabingwa watetezi Madrid msimu huu baada ya ushindi wake wa mabao 4-1 dhidi ya Deportivo Alaves Jumamosi iliyopita.

Kwa ujumla, Benzema amepachika mabao 15 kwenye mashindano yote msimu wa 2020-21.

Benzema amefunga angalau mabao 15 katika misimu 10 kati ya 11 aliyoichezea Madrid katika mashindano yote.

## ZISIKUPITE

### TUCHEL AMTAKA UPAMECANO

KOCHA mpya wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema beki wa klabu ya RB Leipzig na Ufaransa, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22, ni miongoni mwa wachezaji anaowalenga sana. ***(SportBild via Team Talk)***

### SPURS WAMTAKA DI MARIA

KLABU ya Tottenham Hotspur, imewasiliana na kiungo wa kati wa PSG na Argentina, Angel di Maria kuhusu uhamisho wa kwenda London. Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United mwenye umri wa miaka 32, atapatikana kwa uhamisho wa bila malipo mwisho mwa msimu huu. ***(L'Equipe via Talksport)***

### YAJITOSA KWA GARCIA

ARSENAL ina kibarua kigumu cha kushindana na Barcelona katika kumsajili mlinzi wa Manchester City mwenye umri wa miaka 21, Eric Garcia, ambaye anatarajiwa kuondoka kama mchezaji huru mwisho mwa msimu huu. ***(Mundo Deportivo via Express)***

### BENTEKE KUBAKI PALACE

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Christian Benteke mwenye umri wa miaka 30, anatarajiwa kusalia katika Klabu ya Crystal Palace licha ya klabu ya West Bromwich Albion kumnyatia. ***(Sky Sports)***

### PSG YAKOMAA NA DELE

PSG bado inatumai kumsajili kiungo wa kati wa Tottenham na England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, kwa mkopo kwa kipindi chote cha msimu kilichosalia.

### SPURS YAMUWINDA NEUHAUS

TOTTENHAM Hotspur inafikiria kumsajili kiungo mchezeshaji wa Borussia Monchengladbach na Ujerumani, Florian Neuhaus mwenye umri wa miaka 23, kama mtu atakeyechukua nafasi yake Dele Alli. ***(Mirror)***

### RAHMAN KUONDOKA CHELSEA

MLINZI wa kushoto wa Chelsea, Baba Rahman mwenye umri wa miaka 26, anatarajiwa kuwa mchezaji wa kwanza kuondoka katika klabu hiyo tangu kocha, Frank Lampard kufukuzwa. ***(Sport24 via London.Football)***

### PELLISTRI KUONDOKA UNITED

WINGA wa Manchester United, Facundo Pellistri, anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Old Trafford kwa mkopo, huku Club Bruges na Alaves zikimnyatia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 raia wa Uruguay, ambaye alijiunga na 'Mashetani Wekundu' hao kutoka Penarol Oktoba. ***(Goal)***

### SPURS KWA MAKSIMOVIC

KLABU YA Tottenham pia inahusishwa na uhamisho wa beki wa Napoli na Serbia, Nikola Maksimovic mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake utakamilika mwisho mwa msimu huu. ***(Spazio Napoli via Sport Witness)***

HABARI MICHEZO

## Class, Mmalawi watunishiana, kupima uzito

**Mwandishi Wetu**

MABONDIA Ibrahim Class na Dennis Mwale wa Malawi, jana wameingia katika vita ya maneno walipokutana uso kwa uso kwa mara ya kwanza kabla ya pambano lao la kesho lililopewa jina la 'The Rumble in Dar'.

Class na Mwale watazichapa kuwania ubingwa wa mabara wa WBF kwenye ukumbi wa Next Door Arena, Dar es Salaam, pambano litakalotanguliwa na mengine manane.

Leo mabondia hao watapima uzito na afya zoezi litakalosimamiwa na rais wa WBF, Goldberg Howard na kushuhudiwa pia na Scott Farrell ambaye ni ofisa mtendaji mkuu wa Global Boxing Stars (GBS), wadhamini wa pambano hilo, hoteli ya Onomo, Benki ya CRDB na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

Mwale na Class walitambiana jana walipokutana uso kwa uso, Mmalawi akisisitiza kuwa anamheshimu Class ambaye ana rekodi nzuri na ni mzoefu ulingoni, lakini hatarajii rekodi yake ya kutopigwa kuvunjwa na Mtanzania huyo.

"Nitamsambaratisha Class mbele ya mashabiki wake, hilo halina ubishi, nimekuja Tanzania kufanya kazi, nimepambana sana hadi kufikia 'levo' ya kuwa bondia wa kimataifa, ngumi ni maisha yangu naziheshimu," alitamba Mmalawi huyo.

Class alisema haitotokea apigwe katika ardhi ya nyumbani akisisitiza kwamba Mwale amedandia treni kwa mbele, hivyo kitakachomkuta kesho hatakisahau.

Pambano la mabondia hao litashuhudiwa na Kubrat Pulev bondia aliyezichapa na Anthony Joshua hivi karibuni, walipowania mikanda ya ubingwa wa WBA, IBF, WBO na IBO.

Pulev ameambatana na mdogo wake, Tervel atakayezichapa na Vikapita Merero wa Namibia kumsindikiza Class na Mwale alisema pamoja na kwamba hajui ubora wa mabondia wa Tanzania, lakini hamasa aliyoikuta nchini hapa kwenye masumbwi hakuitarajia.

"Tumekuja kufanya kazi, katika familia yetu hatuna pambano kubwa wala dogo, ndiyo sababu mdogo wangu hajawahi kupigwa, na mimi mbali na Anthony Joshua, hakuna pambano nimewahi kupoteza, hivyo tunakwenda kuendeleza historia hiyo katika ardhi ya Tanzania," alijinasibu Pulev.

Mpinzani wao alisema pamoja na kwamba anacheza ugenini, lakini yeye ni Mwafrika na bila shaka hatowaangusha Waafrika wenzake kutoka Tanzania.

# GOFU YA JOHHNIE WALKER YAMALIZIKA KWA KISHINDO

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya gofu maarufu Kombe la Johnnie Walker Waitara 2021, yaliyomalizika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam kwenye viwanja vya Gofu Lugalo na kuhudhuriwa na jumla ya washiriki 180 kutoka ndani na nje ya nchi, yamefanyika kwa kiwango cha juu, imeelezwa.

**Akizungumza katika hafla ya chakula cha jioni iliyoambatana na utoaji wa zawadi kwa washindi, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Venance Mabeyo, alisema mashindano hayo yameendelea kujizolea umaarufu ndani na nje ya nchi kwa kuwavutia wachezaji kutoka sehemu mbalimbali kushiriki.**

Mashindano hayo ambayo hufanyika kila mwaka, yalitarajiwa kuhudhuriwa na jumla ya wachezaji 150 lakini idadi iliongezeka na kufikia 180.

Mabeyo aliishukuru Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), ambayo ilidhamini mashindano hayo kupitia kinywaji chake cha Johnnie Walker na kuyataka makampuni mengine kuiga mfano wa Serengeti ili kuusukuma mbele mchezo wa gofu.

Naye Mkuu wa Majeshi wa Malawi, Jenerali Vincent Nundwe, ambaye alishiriki pamoja na timu yake ya maofisa wa jeshi wa ngazi mbalimbali, aliishukuru Tanzania kuwaalika kushiriki na kusema michezo inasaidia kujenga undugu na kukuza ushirikiano.

"Tunawashuru ndugu zetu wa Tanzania kutualika kushiriki katika mashindano haya makubwa. Tumefurahi sana na pia napenda kuwaomba wanajeshi kushiriki katika michezo kwani pamoja na kujenga afya pia hukuza urafiki na ushirikiano," alisema Nundwe.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema amefurahishwa na ufanisi na maandalizi mazuri ya mashindano hayo na kuupongeza uongozi wa Klabu ya Lugalo kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya.

"Nimefurahishwa na maandalizi mazuri ya mashindano haya. Viwanja vipo katika hali nzuri na pia naamini kila aliyecheza atakuwa amefurahi kucheza kwenye viwanja vizuri nikiwamo mimi mwenyewe," alisema mkurugenzi huyo.

Mark alisema SBL ni mdau wa michezo hapa nchini na kusisitiza itaendelea kudhamini mashindano hayo makubwa yanayofanyika kila mwaka hapa nchini.

SBL pia ndiyo mdhamini mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambayo jana ilicheza mechi yake ya mwisho ya hatua ya makundi kwenye Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) inayoendelea nchini Cameroon, lakini pia kampuni hiyo ndio wadhamini wakuu wa Ligi ya Wanawake Tanzania kupitia bia yake ya Serengeti Lite.

UMETISHA...




Veterani wa mchezo wa gofu, Dk. Edmund Mndolwa (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 1.5 mshindi wa kwanza wa mashindano ya Johnnie Walker Waitara Trophy, Bryson Nyenza, ambaye ni mchezaji wa kulipwa (profesional player) kutoka Klabu ya Gofu ya Lugalo. Mashindano hayo yalidhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti kupitia kinywaji chake cha Johnnie Walker, huku hafla hiyo ikifanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Mgosi aiandalia zawadi Yanga Princess*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema ameandaa zawadi kwa watani wao, Yanga Princess endapo tu watamfunga katika mechi yao ya mzunguko wa pili na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu.

Kauli hiyo ya Mgosi ameitoa juzi baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 11-1 dhidi ya TSC Queens, mechi iliyopigwa Uwanja wa Mo Simba Arena uliopo Bunju, na kwa matokeo hayo wadada hao wa Simba sasa wamepanda hadi nafasi ya pili wakiwa na pointi 29 huku vinara Yanga wakiwa na pointi 31.

Mgosi alisema baada ya kumaliza mzunguko wa kwanza dhidi ya TSC Queens kwa ushindi wa mabao 11-1, sasa wanaenda kujipanga kuhakikisha kila mechi ya duru la pili wanapata pointi tatu muhimu.

Alisema huku akiwaombea Yanga Princess ambayo inanolewa na Edna Lema kuendelea kupata matokeo mazuri kwa sababu anahitaji ubingwa wa ligi hiyo kuamuliwa na mechi ya watani wa jadi katika ligi hiyo ya wanawake.

"Nafurahi kuona Yanga Princess ikifanya vizuri na ninampongeza Edna ambaye ni kocha mwanamke anayeleta ushindani, kwa upande wangu tumejipanga kuhakikisha msimu huu hachukui ubingwa, nitaandaa zawadi ya kumpa kocha wao endapo atanifunga mzunguko wa pili na kutwaa taji hilo.

"Nimpongeze Edna kwa msimu huu kujitahidi kuandaa timu yake ila suala la ubingwa itakuwa ngumu kuchukuwa, hata hivyo ningependa bingwa wa ligi hii kuamuliwa na mechi kati yetu Simba na Yanga ambao wenzetu wametuzidi pointi mbili," alisema Mgosi.

Alisema baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wanaenda kujipanga kwa kuangalia upungufu na walipokosea ili duru la pili kupambana kutafuta pointi tatu.

# Michezo

Alhamisi Januari 28, 2021

Nipashe




HABARI UK.22

## Benzema atarejea Lyon, asema wakala

## Kaze ataja ubingwa, Mghana kumsaidia

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI mabosi wa Yanga wakimleta Edem Mortotsi kuwa kocha wa viungo pamoja na utimamu wa mwili nafasi ambayo ilikuwa wazi tangu kuondoka kwa Riedoh Berdien raia wa Afrika Kusini, Kocha Mkuu wa vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Cedric Kaze, amesema atamaliza hesabu zake za kutwaa ubingwa mapema.

Taarifa kutoka Yanga zinasema tayari Mortotsi aliyekuwa akiichezea klabu ya FC Edmonton ya Canada, ameshatua nchini tangu juzi na sehemu kubwa ya mazungumzo imekwenda vizuri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema amefanya usajili wa malengo katika kipindi cha dirisha dogo na anaamini kasi waliyoionyesha katika mzunguko wa kwanza itaendelea.

Kaze alisema Yanga ina jambo moja tu msimu huu nalo ni kuwavua Simba ubingwa, hivyo akili, mikakati na mipango yao ni kufanya vema katika mechi zote za ligi.

"Tunaendelea vizuri na mazoezi na wachezaji wote wanajua malengo ya timu, kila mmoja anapojiunga na Yanga anajua amekuja kuongeza nguvu, naamini tutatimiza ahadi hii, ingawa hakuna kazi rahisi kwenye mbio hizi," alisema Kaze.

Aliongeza bado hakuna timu yenye uhakika wa kutwaa taji hilo, na kuna timu tatu ambazo anaamini endapo zitafanya vizuri, mojawapo itaibuka bingwa wa ligi.

"Ubingwa hauna mwenyewe, kikubwa sisi tushinde mechi zetu, huwezi kuwa bingwa kama wewe mwenyewe unafanya vibaya, tunajaribu kurekebisha makosa ili ligi itakaporudi tuwe tumeimarika na tayari kupambana," Kaze alisema.

# MORRISON AKERA WAKIIUA AL HILAL

## ●●● Ahoji wanamwambia ana 'kitenesi', atupia mawili Simba ikitakata kwa Mkapa huku...

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI mwenye vituko, Benard Morrison, jana aliwafanya wanachama na mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani na wale waliokuwa wanafuatilia mechi ya Simba Super Cup kuwa na furaha baada ya kufunga mabao mawili peke yake na kutoa pasi ya bao moja wakati akitokea benchi kipindi cha pili, hivyo kuifanya timu yake kushinda 4-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu wa ligi akitokea kwa mahasimu wao wa jadi, Yanga na kuzua mzozo mkubwa ulioamuliwa na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya (TFF), alifunga mabao mawili ndani ya dakika tatu tu baada ya muda mrefu Simba kuwa mbele kwa ikiongoza 2-1.

Dakika ya 86, alichukua mpira pembeni mwa uwanja na kuwalamba chenga mabeki wa Al Hilal kabla ya kuachia shuti la mguu wa kushoto lililokwenda moja kwa moja wavuni na kumuacha kipa Salim Magoola akiwa hana la kufanya, likiwa ni bao la tatu.

Dakika moja kabla ya mechi kumalizika, Morrison tena alichukua mpira katikati ya uwanja na kuupeleka pembeni kwa Mohamed Hussein 'Tshabalala', akauomba tena na kupiga shuti la mbali, lakini la kukata staili ya 'mwezi mwandamo' na kujaa wavuni, akiandika bao la nne na kuwaacha mashabiki wa Simba wakiwa hawajiwezi kwa furaha, akiinogesha michuano hiyo ya Simba Super Cup.

Mashabiki wa Simba walilipuka kwa furaha zaidi baada ya staili yake ya kushangilia bao la kwanza kwa kuchukua mpira na kuingiza ndani ya bukta katikati ya mapaja na kutembea kama mtu mwenye busha ('kitenesi').



**'KITENESI' STAILI...**

Winga wa Simba, Mghana Bernard Morrison, akishangilia kwa staili ya mithili ya mtu mwenye busha kwa kuuweka mpira katikati ya mapaja baada ya kufunga moja kati ya mabao mawili aliyotupia wakati Simba ikishinda 4-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

Akizungumzia staili hiyo baada ya mechi kumalizika, Morrison alisema: "Watu wanasema nina busha, mimi sijui busha ni nini, nilivyouliza nikafafanuliwa kuwa busha ni henia, sasa nilivyosikia hivyo, nikasema alah, henia mbona ni ugonjwa kama ugonjwa mwingine! Kama kichwa kukuuma, mkono na magonjwa mengine.

"Sasa wenyewe wanafikiria henia inashika eneo hilo...pekee yake, mimi nimeweka mpira eneo hilo kwa kuwathibitishia kuwa ndio nina busha," alitania Morrison.

Awali, dakika ya 72, Morrison alifanya shambulizi kwenye lango la Al Hilal kwa kupiga shuti lililotemwa na kipa Mangoola, kabla ya mchezaji mpya wa timu hiyo aliyesajiliwa kutoka FC Platinum, Perfect Chikwende kuukwamisha wavuni akiandika bao la pili.

Mechi hiyo ilianza taratibu, lakini ilikuwa ikichangamka kadri muda ulivyokuwa ukisonga mbele.

Ilikuwa ni dakika ya 38 wakati Bwalya alipoipatia Simba bao la kuongoza baada ya shambulizi lililofanywa na Chikwende, akimpasia Chama, lakini alipiga shuti dhaifu lililombabatiza beki mmoja wa Al Hilal, ukarudi uwanjani na kumkuta mfungaji aliyeachia shuti lililokwenda moja kwa moja wavuni.

Dakika moja kabla ya mapumziko, Al Hilal ilisawazisha bao kupitia kwa Saleem Mohamed kwa kichwa.

Michuano hiyo ambayo ni maalum kwa timu hizo kujiandaa na hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, itaendelea tena kesho kwa Al Hilal kucheza mechi dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo kabla ya Jumapili Simba kuhitimisha na Wakongomani hao.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >